# Nipashe

Ijumaa Agosti 14, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580310

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Ashikiliwa tuhuma za kumuua shemeji yake akiamulia ugomvi

UKURASA 3




UKURASA 11

# Siri uteuzi kinamama ubunge CHADEMA hii

**KATI** ya majimbo 10 Dar, wanaume wawili tu wachomoza, miji mikubwa washinda kura za maoni na kupewa nafasi...

*Endelea ukurasa wa 2*



Asia Msangi - **Ukonga**



Halima Mdee - **Kawe**



Khadija Mwago - **Mbagala**



Lucy Mageleli - **Kigamboni.**



Suzan Lyimo- **Kinondoni**

## Mtaalam ataja sababu matetemeko ya ardhi

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**TCRA YABAINISHA SABABU ZA LUNINGA, REDIO KUOMBA VIBALI**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeeleza sababu tatu za kutaka vituo vya utangazaji nchini vinavyojiunga na vituo...

UKURASA WA 7

**USAFIRI ZIWA VICTORIA SASA KUANZA AGOSTI 16**

SIKU chache baada ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Agosti 9, mwaka huu, kumuagiza Katibu Mkuu wa Wizara...

UKURASA WA 10

**MADEREVA WALIZWA BARABARA RUSUMO**

MADEREVA wa magari ya mizigo kutoka mikoa mbalimbali nchini, wameiomba Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na...

## MHADHIRI KUBURUZWA KORTINI MADAI RUSHWA NGONO

UKURASA 3

**MICHEZO** **MASWALI MAGUMU HUKUMU YA MORRISON** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mtaalamu aeleza sababu ya tetemeko

**Na Romana Mallya**

MJIOLOJIA Mwandamizi na Mkuu wa Kitengo cha Majanga ya Asili kutoka Wakala wa Jiolojia nchini (GST), Gabriel Mbogoni, amesema matetemeko hayatabiriki.

"Linapotokea wananchi wachukue tahadhari kama wapo ndani ya nyumba wabaki ndani na kama wapo nje wabaki nje kusiwe na hali ya kutaharuki," alisema.

Alitoa maelezo hayo kutokana na taharuki iliyowakumba wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine baada ya kupita tetemeko hilo juzi majira ya saa mbili usiku na kudumu kwa sekunde kadhaa.

Baadhi ya wakazi waliokuwa kwenye majengo marefu walikimbilia nje kuhofia usalama wa maisha yao.

Mjiolojia huyo alisema sio mara zote mtikisiko unaweza kufanana kwa sababu inategemea wa kwanza ulitokeaje.

"Kama nguvu ya mwanzo ilikuwa kubwa inaweza isijirudie tena hii inategemeana na namna ambavyo nguvu ilivyojikusanya, kama mtikisiko wa kwanza ulikuwa ndio mkusanyiko pekee haiwezi kujirudia, kama ilikuwa zaidi inaweza kujirudia kwa wiki au miaka," alisema.

Kuhusu ukubwa wake, alisema ma hawezi kuujua na kutoa tahadhari kwa wananchi kuwa tetemeko haliwezi kuzuilika.

"Linapotokea wananchi wachukue tahadhari kama wapo ndani ya nyumba wabaki ndani na kama wapo nje wabaki nje kusiwe na hali ya kutaharuki," alisema.

**TMA YAFAFANUA**

Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), imefafanua kutokea kwa tukio hilo la tetemeko, hakuna tishio la kusababisha mawimbi ya Tsunami baharini.

"Tetemeko hili halikuwa na nguvu kubwa na hakuna maporomoko ya ardhi yaliyotokeza baharini ambayo yangeweza kuzalisha tsunami," ilisema taarifa hiyo.

Mamlaka hiyo ilisema kuwa inaendelea kufuatilia mifumo ya hali ya hewa baharini na kutoa taarifa endapo kutatokeza mwendelezo wa matetemeko katika eneo la bahari.

"Hakuna athari zilizojitokeza au zinazotarajiwa katika mifumo ya hali ya hewa ya bahari kutokana na tetemeko hili," ilisema.

Mamlaka hiyo imewashauri watumiaji wa eneo la bahari ikiwa ni pamoja na wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyo karibu na Bahari ya Hindi kutokuwa na hofu na kuendelea na shughuli zao kwa kuzingatia taarifa ya hali ya hewa baharini kama walivyoitoa awali.

**WANANCHI WASIMULIA**

Baadhi ya wananchi katika mitandao mbalimbali ya kijamii wameeleza walivyokumbwa na tetemeko hilo katika maeneo yao.

Mkazi wa jijini Dar es Salaam, Luis Mbunda alisema wakati tetemeko hilo likitokea alikuwa sokoni Kariakoo na alihisi kama amepatwa na degedege.

Hawa Musa, mkazi wa Mwenge alisema wakati likitokea alikuwa amekaa sebuleni kwake na mtikisiko alioupata alijikuta amekimbilia mtaani kuhofia kudondokewa na nyumba.

Mkazi wa Tabata, John Joseph, alisema wakati likitokea alikuwa njiani kuelekea nyumbani na alipohisi mtikisiko huo alikimbia akidhani ardhi inataka kupasuka ndipo baadaye alipoelezwa lilikuwa ni tetemeko la ardhi.

Baadhi ya wakazi wa Kariakoo ambako majengo mengi ni ya ghorofa, walisema walisikia tetemeko la nguvu na kuhisi nyumba inaweza kudondoka ndipo wakakimbia kushuka chini ya jengo kwa usalama wao.

Kwa mujibu wa mtandao wa Volcano Discovery, Septemba 10, 2016 saa 9:27 mchana kulitokea tetemeko la ardhi mkoani Kagera ambako ni kitovu kwenye makutano ya latitudo 10 06' na longitudo 31055' eneo ambalo ni kilomita 20 Kaskazini Mashariki mwa kijiji cha Nsunga na kilomita 42 Kaskazini Magharibi mwa mji wa Bukoba.

Kitovu hicho kilikuwa kilomita 10 chini ya ardhi kwenye eneo hilo. Nguvu za mtetemo wa ardhi wa tetemeko hilo lilikuwa ni 5.7 kwa kutumia skeli ya "Richter" ukubwa ambao ni wa juu kiasi cha kuleta madhara makubwa.

Kutokana na ukubwa huo maeneo mengi ya Mkoa wa Kagera ikijumuisha mji wa Bukoba yalipatwa na madhara makubwa ikijumuisha nyumba nyingi kupasuka na watu wengi kujeruhiwa kwa kuangukiwa na vifusi na kuta za nyuma ambapo inakisiwa kuwa watu 13 walipoteza maisha yao.

Mwezi Aprili mwaka 2017 tetemeko lingine lenye ukubwa wa 5.7 kwa vipimo vya Richter lililotokea tena na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 10 na kujeruhi watu wasiopungua 200 na kuwaacha mamia bila makazi.

Mwezi Machi, mwaka huu, GST walithibitisha kutokea tetemeko la ardhi saa 3:27 usiku lenye ukubwa wa kipimo cha Richa 4.9, mkoani Tanga.

Mbogoni alisema tetemeko hilo lilidumu kwa sekunde 12 ambapo kitovu chake ni eneo la Vulaya lililopo umbali wa kilometa 19 kutoka Maramba, Korogwe mkoani humo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipewa maelezo ya Kivuko cha Mafia, alipokagua ujenzi wake unaofanywa na Kampuni ya Songoro Marine, Kigamboni jijini Dar es Salaam, jana. Kivuko hicho, kitakapokamilika kitafanya safari kati ya Kisiwa cha Mafia na Nyamisati mkoani Pwani. **PICHA: OWM**

# Siri uteuzi kinamama ubunge CHADEMA

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetangaza orodha mpya ya wagombea ubunge wake, huku jijini Dar es Salaam kukitawaliwa na safu ya kinamama.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa CHADEMA, Tumaini Makene, katika orodha hiyo mpya ya wagombea ubunge 37 wa Tanzania Bara aliyoitoa jana, wamo kinamama 11. Kati yao, wamo watatu wanaofanya idadi ya wagombea wanawake Dar es Salaam kufikia watano.

Kwa mujibu wa Makene, chama hicho hakijateua wagombea katika majimbo Kibamba, Temeke na Ilala jijini kutokana na sababu mbalimbali.

Makene alibainisha kuwa, Temeke na Ilala ni miongoni mwa majimbo saba ambayo chama hicho kitalazimika kurudia mchakato wa kura za maoni wakati Kibamba ni miongoni mwa majimbo saba ambayo CHADEMA haijapiga kura za maoni kuwapata wagombea wake.

Makada wanaume waliochomoza katika uteuzi huo wa CHADEMA jijini Dar es Salaam ni aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, anayewania ubunge wa Ubungo na John Mrema, anayesaka ubunge wa Segerea.

Vilevile, taarifa za chama hicho zinaonyesha kuwapo kwa wateule wengi wanawake wanaopeperusha bendera ya CHADEMA katika majimbo ya miji mikubwa, ikiwamo Shinyanga Mjini, Mpanda Mjini, Morogoro Mjini, Tarime Mjini, Geita Mjini, Bunda Mjini na Tabora Mjini.

Orodha ya kwanza iliyotolewa Jumapili na Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kigaila, ilionyesha mageuzi ya kinamama kuchomoza wakiwa jumla ya wateule 40 kati ya 163.

Katika orodha iliyotolewa jana, wanawake waliochomoza katika majimbo ya Dar es Salaam ni Susan Lyimo (Kinondoni), Khadija Mwago (Mbagala) na Lucy Magereli (Kigamboni).

Makada wanawake wa CHADEMA waliokuwamo kwenye orodha ya kwanza ya wateule wa chama hicho kuwania ubunge majimbo ya Dar es Salaam ni Asia Msangi (Ukonga) na Mwenyekiti wa Wanawake wa chama hicho (BAWACHA), Halima Mdee anayewania tena ubunge wa Kawe.

**SIRI KINAMAMA KUTAMBA**

Alipoulizwa na Nipashe jana kuhusu siri ya wanawake kung'ara katika uteuzi wa wagombea ubunge mwaka huu kupitia chama hicho, Makene alianika sababu mbili.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, sababu ya kwanza ni mkakati wa muda mrefu wa chama hicho kuandaa viongozi, ambao alidai umekumbwa na misukosuko mingi ikiwamo kufuatiliwa na vyombo vya dola.

Makene aliitaja sababu ya pili kuwa ni programu mahsusi ya BAWACHA kuhamisha wanawake kujitosa katika uongozi, akifafanua kwamba, "siyo jambo la kubahatisha, liliandaliwa kwa muda mrefu na viongozi wa BAWACHA wamekumbana na mengi, ikiwamo kupigwa mabomu."

Taarifa ya jana ya Makene ilibainisha kuwa Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii, Lazaro Nyalandu, aliyeshika nafasi ya pili katika kura za maoni kumsaka mgombea urais kupitia chama hicho, atagombea ubunge wa Singida Kaskazini.

Mbali na kinamama waliong'ara katika uteuzi wa majimbo ya Dar es Salaam, orodha ya jana ya CHADEMA ilikuwa na majina ya Jacqueline Swai (Ngorongoro), Khadija Madwanga (Kwimba), Neema Chozaile (Geita Vijijini), Salome Makamba (Shinyanga Mjini), Jedidia Kitundu (Msalala), Aisha Madoga (Dodoma Mjini), Hadija Maula (Mvumi) na Cecillian Ndossi (Monduli).

Wengine ni Joel Hema (Singida Mashariki), Martin Mussa (Tabora Kaskazini), Gibson Ole-Meiseyeki (Arumeru Magharibi), Gervas Sulle (Mbulu Mjini), Aboubakar Mashambo (Bumbuli) na Norbeet Marandu (Handeni Mjini).

Vilevile, Nicholous Mapunda (Peramiho), Renatus Nzemo (Bukombe), Gody Bagamba (Mbogwe), Adolf Mkono (Karagwe), Thedo Assechekamwati (Kahama), Emmanuel Magema (Ushetu), Idd Amri (Kishapu), Edson D'zombe (Lupembe), Frederick Kihwelo (Mafinga Mjini), Emmanuel Lusambo (Mpanda Vijijini), James Lembileki (Ludewa) na Peter Mdidi (Mvomero).

Pia wamo Issa Chilindima (Newala Mjini), Arfat Kadewele (Tunduru Kusini), Marato Marwa (Butiama), Larazo Maige (Uliyankulu), Philbert Macheyeki (Urambo) na Nyenje Undi (Tunduru Kaskazini).

Orodha hiyo ya jana ilifanya jumla ya wagombea walioteuliwa na CHADEMA kuwania ubunge kufikia 200. Tanzania ina majimbo ya uchaguzi 264. Kati yake, 214 yako Tanzania Bara na 50 yako Zanzibar 50.

HABARI KITAIFA

# Ashikiliwa madai ya kumuua shemeji yake

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro, linamshikilia Shinje Njilangila (30), mkazi wa Kijiji cha Mbamba, wilayani Kilosa kwa tuhuma za mauaji ya shemeji yake Dotto Ngembe (28), kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Agosti 12 baada ya Ngembe kuingilia mgogoro wa kimahusiano uliozuka baina ya mtuhumiwa na mkewe, Kulwa Ngembe, ambaye ni dada wa marehemu.

Kamanda Mtafungwa alisema mauaji hayo yalitokea nyumbani kwa marehemu ambaye alikuwa amewaita wanandoa hao kwaajili ya kusuluhisha ugomvi uliokuwa ukiendelea baina yao, ndipo mtuhumiwa alipomshambulia shemeji yake hadi kumsababishia umauti.

"Chanzo cha tukio hili mtuhumiwa alimfuata mkewe nyumbani kwa shemeji yake kwaajili ya usuluhishi, lakini ilipofika majira ya saa sita usiku ndipo alipofanya mauaji kwa kaka wa mke wake aliyekuwa akimtuhumu kuwa ndio chanzo cha mgogoro wao na baada ya kutekeleza mauaji hayo alikimbia mafichoni," alisema Mtafungwa.

# Mhadhiri kufikishwa kortini kwa tuhuma rushwa ngono

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na Ofisi ya Mashtaka, inatarajia kumfikisha mahakamani Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Jacob Nyangusi (43), kwa tuhuma za kutaka rushwa ya ngono.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema mtuhumiwa huyo alikutwa na TAKUKURU majira ya saa 3:00 Oktoba 3, 2018 nyumbani kwake, eneo la Nyumba 300.

Alisema TAKUKURU ilimkamata mtuhumiwa huyo kabla hajatenda nia ovu ya kufanya ngono na mwanafunzi wake wa mwaka wa kwanza wa Shahada ya Sanaa katika Jiografia na Mazingira.

"Tumemfungulia shauri Nyangusi kwa tuhuma za kutaka rushwa ya ngono kinyume cha kifungu cha 25 cha Sheria ya Kupambana na Rushwa namba 11/2007," alisema Kibwengo.

Kibwengo alisema awali, TAKUKURU ilipokea taarifa kwamba mtuhumiwa alimtaka mwanafunzi wake kingono ili kumsaidia mitihani ya marudio na kumwezesha kufaulu na ndipo ikaweka mtego na kumkamata.

Kibwengo alisema kwa kushirikiana na Ofisi ya Mashtaka imewafikisha mahakamani Theobald Maina (44) aliyekuwa Diwani wa Kata ya Ntyuka jijini hapa, Benedict Mazengo (60) ambaye ni ofisa mtendaji na Anderson Jonathan aliyekuwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Chimala.

Wote hao, alisema wanashtakiwa kwa makosa ya matumizi mabaya ya mamlaka kinyume cha kifungu cha 31 na ubadhirifu kinyume na kifungu cha 28 vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007.

Kibwengo alisema uchunguzi umeonyesha kwamba Aprili, 2016 watuhumiwa kwa pamoja walitumia vibaya madaraka yao, hivyo kujipatia kwa njia ya kughushi Sh. Milioni mbili ambazo ni malipo ya minara ya simu iliyoko kwenye Kata ya Ntyuka.




# Mahakama yamwamuru Lissu kufika mahakamani

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemwamuru kufika mahakamani mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu na wenzake watatu, wanaokabiliwa na kesi ya uchochezi, Septemba 14, mwaka huu, baada ya jana kushindwa kufika kusikiliza kesi yake.

Amri hiyo ilitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai shauri lilipangwa kwa kutajwa na kwamba mshtakiwa Lissu, hakufika kusikiliza kesi yake.

Mdhamini wa Lissu, Robert Katula, alidai mshtakiwa aliwasiliana naye juzi asubuhi na kumueleza kwamba yuko mkoani anatafuta wadhamini kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka huu.

Hakimu Simba, alimtaka mdhamini huyo kuhakikisha mshtakiwa anafika mahakamani na sio kutoa sababu ambazo sio za kisheria.

"Mdhamini hizo sababu hazikubaliki kisheria tusiikosee sheria, sisi ni watekelezaji wa sheria ambapo tunatoa amri. Ukisema unaiachia mahakama tunaweza kusema ulipe dhamana na ukishindwa unakwenda jela hatutaki kufika huko, wewe hakikisha unamleta mshtakiwa tarehe ijayo," alisema.

Hata hivyo, wadhamini wa Lissu waliomba mahakama kujitoa katika udhamini kwasababu wanayemdhamini hana ushirikiano mzuri na wadhamini wake na mahakama iliwaeleza kuwa kisheria mdhamini akitaka kujitoa lazima kwanza anamleta mshtakiwa halafu ndiyo aweze kujitoa.

Kwa upande wa mshtakiwa wa tatu ambaye hakufika mahakamani Mehbooh, ilidaiwa na mdhamini wake kuwa ni mgonjwa na kuwasilisha fomu mahakamani hapo.

Hakimu Simba baada ya kusema hayo, alimtaka mdhamini wa Lissu ahakikishe mshtakiwa huyo anafika mahakamani hapo tarehe ijayo na sio vinginevyo.

Mbali na Lissu washtakiwa wengine ni, Wahariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na Mchapishaji wa Kampuni ya Jamana, Ismail Mehbooh.

Katika kesi ya msingi kwa pamoja washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume na Sheria ya Magazeti ya Mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016 jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari kisemacho, 'Machafuko yaja Zanzibar.'

Katika shtaka la pili wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016 walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar.

Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13 ,2016 katika jengo la Jamana lililopo Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.



Kijana akikinga petroli kwenye gari la kubebea mafuta, lililokuwa kwenye foleni katika barabara ya Mandela, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake na chombo hicho, kwani anaweza kusababisha milipuko. **PICHA: CHARLES MLEO/ TUDARCO**

# Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Bukoba, imewahukumu kunyongwa hadi kufa washtakiwa watatu katika matukio mawili ya mauaji na kumwachia huru mmoja miongoni mwao

Akitoa hukumu ya kwanza inayohusu mauaji, maarufu kama ukataji wa makoromeo, Jaji Sam Rumanyika alisema Aliyuu Dauda na Rashid Athuman, walifanya mauaji ya kukusudia Mei 9, 2015 Kata ya Kitendagulo Manispaa ya Bukoba.

Jaji Rumanyika alisema mtuhumiwa wa kwanza, Dauda, alijihusisha na mauaji ya Herman Grid huko Kitendagulo kwa kumkata koromeo.

Pia alisema mtuhimiwa Athumani alikiri kujihusisha na matukio ya uchomaji wa makanisa. Jaji Rumayika alisema katika shauri la jinai namba 79/2016, mshitakiwa Shija Bunzali alifanya mauaji ya aliyekuwa Diwani wa Kimwani Wilaya ya Muleba kwa tiketi ya CUF, Sylvester Faustine, Januari 31, 2016.

Alisema mtuhumiwa huyo amehukumiwa kifo baada ya kukiri kuwa vifaa vilivyoko kwake vilivyonekana kuwa na damu ni mali yake.

"Mshtakiwa alikutwa na panga likiwa na damu mbichi na suruali aliyosema ni mali yake ikiwa na tone la damu, kwani taarifa ya vinasaba inatoa vielelezo hivyo," alisema Jaji Rumanyika

Alisema watuhumiwa wawili wa uchomaji makanisa na mauaji wameonekana kuwa na makosa katika kesi ya jinai namba 34/2020 na mtuhimiwa wa tatu kuonekana kuwa na hatia katika shauri la jinai namba 79/2016.

Jaji Rumanyika alisema watuhumiwa hao wawili walikiri mbele ya mlinzi wa amani kuwa ushahidi uliotolewa ulijitosheleza kuwatia hatiani. Ushahidi huo, alisema ulitolewa na ofisa wa polisi.

"Ushahidi uliotolewa na upande mashkata unajitosheleza kuwatia hatiani kwani mashahidi wa watuhumiwa walikuwa watano akiwamo ofisa wa polisi na itoshe kusema kuwa mahakama haiwezi kumtia hatiani mshtakiwa wa upande mmoja tu," alisema.

Katika hatua nyingine, Jaji Rumanyika alimwachia huru Ngesela Keeya baada ya vielelezo vya mahakama kutoonyesha kuwa na kosa.

## TCRA yabainisha sababu za luninga, redio kuomba vibali

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeeleza sababu tatu za kutaka vituo vya utangazaji nchini vinavyojiunga na vituo vingine vya kanda, nje ya nchi na raia wa kigeni kuwatembelea kupata kibali kabla ya kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa kwenye gazeti hili jana, na Mkurugenzi Mkuu, lazima hiyo inatokana na mabadiliko ya kanuni ya 37, zinazoruhusu vituo vya utangazaji kujiunga na kituo chochote cha utangazaji kwa ajili ya matangazo mubashara ili mradi kunakuwa na makubaliano ya kibiashara.

Lengo ni kuweka uwazi madhumuni ya ushiriki wa raia wa kigeni katika shughuli za utangazaji wanapotembelea vituo vya utangazaji nchini.

Pia, kutimiza matakwa ya itifaki za kidiplomasia kuwa wawakilishi wa nchi za nje na mashirika ya kimataifa wanapaswa kuambatana au kupokewa kule wanapokwenda na maofisa wa serikali wanapokuwa wamepata kibali cha kutembelea miradi ambayo wanajihusisha nayo.

Kadhalika, kuhakikisha uendeshaji wa vituo vya utanagazaji unazingatia udhibiti wenye uwazi hususan kwa upande wa ufundi, ujenzi wa vituo hivyo huruhusiwa kwa kibali.

Aidha, vituo hivyo vimetakiwa kuwasilisha maombi ndani ya siku saba tangu kutolewa kwa taarifa hiyo Agosti 11, mwaka huu.

Alifafanua kuwa utaratibu huo ni wa kawaida wenye lengo la kuleta ufanisi katika usimamizi wa maudhui yanayorushwa na vituo hivyo.

TCRA ilieleza kuwa uzoefu uliopatikana katika kusimamia utekelezaji wa kanuni hiyo, kumekuwa na changamoto ya vipindi au habari zinazorushwa na vituo vya utangazaji vinapojiunga na vituo vya nje ya nchi na kurusha habari au matukio nchini.

"Kwa mfano inapotokea dhahiri kuwa habari zinazohusu nchi yetu hazikuzingatia maadili na weledi wa uandishi wa habari, huku habari hizo zikirushwa na vituo vilivyopewa leseni na TCRA, ni dhahiri inasababisha changamoto katika utekelezaji wa kanuni hizo," alisema.

Alisema kutokana na mazingira hayo, ututuzi marekebisho ya kanuni ya 37 yamefanyika kwa kuongeza kifungu kidogo cha 2 iliyotaka kituo chochote cha utangazaji kinachojiunga na kituo kingine cha ndani au nje ya nchi kwa ajili ya kurusha matangazo yake yakiwamo ya mubashara kupata kibali/ruhusa ya kufanya hivyo kutoka TCRA.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, marekebisho hayo yanavihusu vituo vyote vya utangazaji vya redio na televisheni na watoa huduma za maudhui mtandaoni.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

# TAARIFA KWA UMMA

## KUANZISHWA KWA MFUMO WA UWASILISHAJI RITANI ZA KODI KWA NJIA YA KIELETRONIKI

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA au Mamlaka) inapenda kuutarifu umma kuwa imeanzisha mfumo wa uwasilishaji wa ritani za kodi kwa njia ya kielekroniki **(E-Filing System)**. Mfumo unapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka **(wwww.tra.go.tz)** kwa kubonyeza sehemu iliyoandikwa Online Tax Return Filing. Mfumo huu umeanzishwa kwa lengo la kuongeza tija katika usimamizi wa kodi kwa kuboresha uwasilishaji wa ritani na hivyo kupunguza gharama kwa upande wa mlipakodi.

Mfumo huu umeanza kutumika rasmi kuanzia **tarehe 6 Agosti, 2020.** Pamoja na ritani za Kodi ya Ongezeko la Thamani zinazowasilishwa kwa njia ya mtandao, mfumo huu mpya utahusisha ritani zifuatazo:

- **Ritani ya makadirio ya Kodi ya Mapato kwa watu binafsi;**
- **Ritani ya makadirio ya Kodi ya Mapato kwa taasisi;**
- **Ritani ya kodi ya Mapato kwa watu binafsi;**
- **Ritani ya kodi ya Mapato kwa taasisi;**
- **Ritani ya tozo ya uendelezaji ufundi stadi/Skills Development Levy (SDL); na**
- **Taarifa ya kodi ya zuio katika mapato ya waajiriwa (PAYE).**

Hata hivyo, wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara ya uchimbaji wa madini, mafuta au gesi wataendelea kuwasilisha ritani zao za kodi ya mapato kwa utaratibu wa sasa kwa kuwasilisha ritani husika katika ofisi zetu za TRA. Vilevile, ritani nyingine ambazo hazijatajwa hapo juu zitaendelea kuwasilishwa kwa njia ya kawaida.

Ritani za Kodi ya Mapato za kuanzia Mwaka wa Mapato 2019 ***(ambazo bado hazijawasilishwa)*** zinatakikwa kuwasilishwa kwa njia ya kielektroniki. Vilevile Ritani za Kodi ya Uendelezaji Ufundi Stadi (SDL Returns) pamoja na taarifa za makato ya kodi ya zuio kwa waajiriwa (PAYE) za ***kuanzia mwezi Agosti 2020*** ambazo muda wa ulipaji wake wa kodi ni kabla au ifikapo tarehe 7 Septemba 2020 zitawasilishwa kwa njia ya kielektroniki.

Mfumo huu utawawezesha walipakodi kupata hati za makadirio ya kodi ***(Tax Assessments)*** mara tu baada ya mchakato wa uwasilishaji kukamilika. Malipo yote ya kodi yanatakiwa kufanywa kwa kutumia ***namba za kumbukumbu za madeni (Tax Debit Numbers)*** zilizopo katika hati za madai.

Mfumo huu wa uwasilishaji wa ritani za kodi kwa njia ya kieletroniki unaambatana na miongozo na mafunzo kwa walipakodi na wadau mbalimbali ili kujenga uwezo wa namna sahihi ya kutumia mfumo huu. TRA inawasihi walipakodi na wadau wengine kufuatilia kwa karibu miongozo itakayotolewa kwa njia mbalimbali za mawasiliano pamoja na kushiriki mafunzo ya namna ya kutumia mfumo huu.

**Kwa maelezo zaidi;**
**Tembelea ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania iliyo karibu nawe**
**Tovuti: www.tra.go.tz**
**Simu bure: 0800 750 075 au 0800 780 078**
**WhatsApp: 0744 23 33 33**
**Barua pepe: huduma@tra.go.tz**
**services@tra.go.tz**

215858102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Corona iwe chachu ya kuboresha sheria, ajira

**KUWAPO** kwa maradhi ya COVID 19 yaliyoanzia China na kusambaa dunia nzima mwaka huu kumeathiri uchumi na sekta nzima ya kazi na kusababisha kuwapo na changamoto kubwa kwenye ajira na wafanyakazi wengi kuyumba kimaisha kutokana na kukosa kazi bila kutegemea.

Mathalani, nchini Marekani takribani watu milioni 20 hawana ajira kufuatia mlipuko wa COVID- 19 uliolazimisha waajiri kusimamisha uzalishaji kufunga viwanda na kampuni , kutoa likizo bila malipo, kupunguza mishahara na wengine kufukuza wafanyakazi.

Wakati corona iliporipotiwa nchini Machi 17, 2020 wafanyakazi na katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji walianza kuona changamoto za maradhi hayo zilizoambatana na hofu ofisi, kampuni na viwanda vikifungwa, kufanyakazi kwa zamu (shifti), kupunguziwa mishahara, kupunguza wafanyakazi na kazi nyingine kufutwa.

Changamoto hizo zinaleta fikra mpya kuwa taifa linahitaji sheria ya namna ya kukabiliana na athari hizo iwapo litaibuka gonjwa kama COVID -19 ambalo linaathiri waajiri, wawekezaji na wafanyakazi kwa muda mrefu.

Mwanzoni mwa wiki hii Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) Dar es Salaam , imeshauri Tanzania kufanya mapitio ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na kuangalia uwezekano wa kuweka kipengele cha namna ya kukabiliana na milipuko na magonjwa hatari ya kuambukiza ili kupunguza athari na changamoto zinazowakumba waajiri na wafanyakazi.

Ni mambo yanayoibuliwa katika jukwaa la kitaifa la vijana, ajira na kazi zenye staha na kuonekana kuwa wakati wa corona mambo mengi yanayohusu ajira yalifanyika bila kuzingatia haki wala ushirikishwaji wafanyakazi ambao walipokea uamuzi bila kuhusishwa.

Wapo waliofukuzwa kazi, kupunguziwa mishahara, wengine hawakulipwa na hata baada ya kurudishwa kazini hakuna malipo ya fidia . Yote hayo yamesababishwa na uamuzi kufanyika bila kuwa na majadiliano ya utatu yakishirikisha vyama vya wafanyakazi, serikali na waajiri.

Tunajua miongoni mwa wafanyakazi waliuomia zaidi ni walimu wa shule au taasisi za elimu za watu binafsi. Wengi hawakulipwa mishahara na wala kujali hatima zao.

ILO inashauri taifa lijifunze changamoto za corona na jinsi zilivyoathiri sekta ya ajira na kuweka kipengele cha namna ya kukabiliana na matukio ya magonjwa hatari ya kuambukiza kwenye Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.

Ni wazi maradhi hayo yalileta usumbufu kwa waajiriwa na kwa waajiri pia kwani wapo waajiri waliolazimishwa kufunga kazi na kuondoka chini ya usimamizi wa polisi. Hasa Zanzibar, huko wenye migahawa na hoteli walilazimishwa kufunga huduma bila kujali bidhaa zitaharibika na gharama zilizolipwa awali na wateja mbalimbali wamiliki waitalazimika bila kujali walikuwa walipata hasara au faida. Sheria hiyo itazungumzia masuala ya fidia nyakati za majanga kama hayo.

Tunaona kuwa kukiwa na kipengele hicho, waajiri, waajiriwa na serikali watakuwa pamoja kujadiliana na kufanya maamuzi sahihi hivyo kupunguza usumbufu baina ya pande zote tatu.

Aidha, ikumbukwe kuwa mafanikio katika sekta ya ajira na uajiri yatawezekana tu iwapo kutakuwa na kazi za staha zinazoheshimu , kukubaliana, kutii na kufuata sheria, sera na mikataba ya kazi ili Watanzania wafanye kazi zenye staha.

Mambo ya ajira yatafanikiwa kwa kuwa na sera na sheria zinazoheshimu na kuendeleza haki za wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kupewa mikataba, kulipwa mishahara inayostahili, haki za likizo, matibabu , malipo ya mafao ya uzeeni na kuendeleza usawa wa kijinsia bila kudhalilisha wanawake na wasichana wala kuwatenga wenye ulemavu katika ajira.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmin Protace

# Elimu kujikinga na rushwa ngono izame zaidi shuleni

**RUSHWA** ni neno kubwa, lenye alama chafu katika jamii ambalo limekuwa likizungumzwa katika maeneo mbalimbali yanayoizunguka jamii iliko katika makazi yao.

Ndani ya msamiati na nadharia pana ya rushwa, kuna aina inayohusishwa na eneo la jinsia- rushwa ya ngono. Mtu anapewa upendeleo wa kupatiwa kitu, kwa mbadala wa ngono isiyo na hiyari.

Licha ya rushwa mara nyingi kuzoeleka kufanyika katika mazingira ya faragha, kuna aina hiyo inayohusiswa na ngono, watu wachache sana wamekuwa wakithubutu hata kulizungumzia.

Hapo ndipo wadau wa haki, waliandaa kilichoitwa Semina za Maendeleo ya Jamii (GDSS) inayoandaliwa na asasi ya TGNP Mtandao, ikiwalenga wanafunzi na wazazi wao, kujadili na kuzungumzia kwa kina rushwa hiyo ya ngono, namna wanavyokutana nazo au kuzikabili.

Bibie Msumi, Mwanasheria, Mchunguzi, pia Mwendesha Mashtaka kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) , jijini Dar es Salaam, anayetoa elimu hiyo, alianisha rushwa hizi katika makundi kama; rushwa ya ngono, rushwa ya madaraka na rushwa ya matumizi mabaya ya ofisi.

Anasema rushwa ya ngono inaweza kufanywa na pande zote mbili, mwanaume kumtaka mwanamke kimapenzi au mwanamke kumtaka mwanaume kimapenzi. Hiyo inatokana na kufanya jambo kwa ajili ya kujifurahisha kama shukrani.

Mwanasheria huyo anasema, rushwa ya madaraka inasababisha hata maendeleo ya sehemu hiyo kuyumba kutokana na usimamizi

**Anasema rushwa ya ngono inaweza kufanywa na pande zote mbili, mwanaume kumtaka mwanamke kimapenzi au mwanamke kumtaka mwanaume kimapenzi. Hiyo inatokana na kufanya jambo kwa ajili ya kujifurahisha kama shukrani.**

wake unakuwa mbovu.

Katika rushwa ya matumizi mabaya ya ofisi, huwa inatumiwa na baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu, ni aina ya upotoshaji dhidi ya gharama za matumizi yanayoendelea katika ofisi zao.

Unaagukia mfano wa kuwapo wanaoenda safari kwa njia mbadala na ili kuhifadhi pesa za usafiri, anaghushi tiketi za safari yake, tena huenda ni ya bei kubwa zaidi.

Mambo ya namna hayo yanakabiliwaje? Anatoa jibu kupitia kwamba katika kupambana na rushwa, ni wajibu wa jamii kutoa taarifa TAKUKURU kupitia namba za simu waazogawa, kuwezesha kuwanasa wahusika wachukuliwe hatua. Mwanasheria huyo anawakumbusha wanajamii, kuwa kila mmoja ni mlinzi wa sehemu husika, hivyo inapotokea anaona kuna mambo ya rushwa, ana wajibu wa kutoa taarifa kwa mamlaka husika.

Mshiriki anayejitambulisha kwa jina, Ally Juma, anasema yeye hakujua kuwapo aina ya rushwa ya matumizi mabaya ya ofisi na madaraka, hivyo kwa faida ya umma wa walio na upeo aliyokuwa nao, anashauri elimu itolewe na ikiwezekana kuwekwe mabango, ili jamii yote ifahamu hayo.

Aidha, mwanafunzi wa shule moja ya sekondari ya kata, jijini Dar es Salaam, anasema rushwa ipo shuleni kwao, kutokana na wanafunzi wa kike wanapofanya mitihani vibaya na kupata alama za chini,wanakutana na magumu kutoka kwa walimu wa kiume.

Anasema, pia mwanafunzi anapochelewa kufika shule, hata kwa bahati mbaya, huagukiwa na adhabu nzito kutoka kwa walimu wa kiume, hata kujenga mazingira ya kukakatisha tamaa kimasomo.

HABARI KITAIFA

# Usafiri Ziwa Victoria kuanza Agosti 16

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SIKU chache baada ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Agosti 9, mwaka huu, kumuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Leonard Chamuriho, kuhakikisha kibali cha meli ya New Victoria Hapa Kazi Tu, kinapatikana ndani ya siku mbili, hatimaye kimetolewa na meli hiyo itaanza huduma kwa wakazi wa Mwanza na Bukoba, Jumapili hii.

Ratiba hiyo ilitangazwa rasmi Agosti 12, mwaka huu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa huduma za meli, Eric Hamissi. Alisema, meli hiyo yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 200 za mizigo, itakuwa ikifanya safari za Mwanza kuanzia saa 3:30 usiku kupitia Kemondo ikielekea Bukoba na kufika saa 12:00 kamili asubuhi, mkoani Kagera.

Eric alisema katika hatua hiyo pia meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu, yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 100 za mizigo, itaanza safari zake rasmi tarehe itakayotajwa na itatoka Mwanza kuelekea kisiwani Ukerewe.

"Meli hizo mbili zitaanza safari zake rasmi, kufuatia kukamilika kwa ukarabati na tayari zimeishakaguliwa na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), kupewa vyeti vya ubora, baada ya mkandarasi KTMI Co. Ltd., ya Korea Kusini kumaliza shughuli hiyo, ambayo imegharimu Sh. bilioni 27.61 ikiwa ni fedha zilizotolewa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100," alisema Eric.

Kuanza kwa safari ya meli hizo kutasaidia kupunguza kwa adha za gharama za usafiri ikiwa na punguzo la bei ya ubebaji wa mizigo na tani moja mteja atalipa Sh. 27,000, Meli ya New Victoria ambayo itakuwa na madaraja matatu tiketi zitauzwa kwa Sh. 16,000 kwa daraja la uchumi, daraja la biashara 30,000 na daraja la kwanza 45,000, huku meli ya New Butiama ambayo itakuwa na madaraja mawili tiketi zikiuzwa kwa Sh. 8,000 kwa daraja la uchumi na 10,000 daraja la biashara.

"Meli ya New Victoria ilisimama kutoa huduma ya usafiri tangu Desemba 2014, kwa sasa itakuwa ikifanya safari zake mara tatu kwa wiki kutoka Bandari ya Mwanza Kaskazini kila siku ya Jumapili, Jumanne na Alhamisi saa 3:30 usiku na kuwasili siku inayofuata alfajiri katika Bandari ya Bukoba kupitia Kemondo," alisema Eric.

Vile vile, kuhusu Meli ya New Butiama, kwa sasa itakuwa ikiondoka Bandari ya Nansio kila siku saa 2:00 asubuhi na kuwasili Mwanza saa 4:00 asubuhi na ita ondoka Mwanza saa 9:00 alasiri, itafika Nansio 11:00 jioni.

# IGP Sirro aridhishwa ujenzi wa bweni la polisi

**Romana Mallya na Fatma Mtutuma**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, amesema ameridhishwa na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bweni la polisi katika Chuo cha Maofisa wa Polisi, jijini Dar es Salaam.


Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Makao Makuu ya jeshi hilo, IGP Sirro alifanya ziara katika Bohari Kuu ya Polisi iliyopo barabara ya Kilwa pamoja na kutembelea chuo hicho cha taaluma ya polisi.

IGP Sirro alisema miradi hiyo inaendelea vizuri na thamani ya fedha iliyotumika inaonekana.

"Miradi hiyo iliwezeshwa na Rais John Magufuli ili Jeshi la Polisi lifanye kazi kwa weledi na kujitegemea," alisema.

IGP Sirro aliwapongeza wasimamizi wa miradi hiyo ambayo kwa sasa imefikia hatua ya mwisho kukamilika kwake.

Rais Magufuli alitoa Sh. milioni 700 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa mabweni ya askari wanafunzi na Sh. milioni 600 kwa ajili ya kiwanda cha ushonaji huku madarasa ya chuo cha utabibu fedha zake zikitolewa na jeshi hilo.



Mamalishe akiandaa chakula kwaajili ya wateja wake, kwenye mazingira machafu katika kona ya Barabara ya Sewa, eneo la Viwandani, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya za walaji. **PICHA: NASRI MCHEKENJE/TUDARCO**

# NMB yamkabidhi Samia vyoo 10 vya shule

**Na Mwandishi WETU**

MAKAMU wa Rais, Samia Suhulu Hassan, amepokea msaada wa matundu 10 ya vyoo vya Shule ya Msingi Kibuteni Kusini Unguja, vilivyojengwa na Benki ya NMB.

Msaada wa vyoo hivyo ni sehemu ya shamrashamra ya Tamasha la Kizimkazi maarufu kwa jina la Kizimkazi Day.

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Dar es Salaam na Unguja, Donatus Richard, amesema msaada huo uligharimu Sh. milioni 10, unawalenga walimu na wanafunzi wa jinsia zote kwa lengo la kuhakikisha wanasoma katika mazingira salama kiafya.

"Hivi vyoo vipo katika ubora wa hali ya juu, lengo ni walimu kutoa elimu nzuri na wanafunzi kupata na kuishi katika mazingira yaliyosafi kwa afya zao." Donatus alisema NMB inaifikia jamii kivitendo na lengo la benki hiyo ni kuwafikia wananchi wote hususani kinamama wajasiriamali ambao bado wamekuwa na muamko mdogo juu ya utunzaji Fedha kupitia mfumo wa kibenki.

"Hatuishii Kizimkazi pekee, Ila tumekuwa tukitoa huduma ya elimu kwa kinamama hususani vikundi vya wajasiriamali maeneo mbalimbali Unguja na Pemba, na hata Tanzania Bara, ambapo tunawashawishi kujiunga na mfumo wa kibenki rahisi kabisa wa Pamoja Account."

"Tunatoa elimu hata kwa mmoja mmoja ambaye ni mjasiriamali, na tunatoa mikopo kwa wafanyabiashara mmoja mmoja, lengo ni kusaidia biashara zao zikuwe kimalengo," alisema Donatus.

Hata hivyo, alisema bado NMB itaendelea kuangalia na kutatua changamoto zilizopo ndani ya jamii katika maeneo yote ya Zanzibar na Bara ambapo kiasi cha asilimia moja ya mapato yake yatanufaisha jamii.

"Sisi lengo letu ni jamii tunayofanya nayo kazi inanufaika na benki yao, kwa kuwa sisi tunapata faida kidogo hatuwezi tumia faida hiyo pekee yetu,".

Kwa upande wake, Samia alishukuru benki hiyo kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele hasa kusaidia kwenye mahitaji muhimu ya jamii.

Naye Meneja NMB Zanzibar, Unguja na Pemba tawi la Mwanakwerekwe, Malindi na Chakechake, Abdullah Duchi, alisema wataendelea kushirikana na wananchi katika mambo mbalimbali ya kijamii kwa lengo la kutatua changamoto zinazowakabili. "Jana tumeshiriki siku ya vijana, katika mambo mbalimbali yakiwamo ya kifedha kuwasaidia wapatapo mikopo iwasaidie kimalengo na tumeanzisha program maalum kwa ajili hiyo 'Chipukizi Program'

Benki ya NMB imekuwa mdau wa karibu wa Tamasha la Kizimkazi Day lililoanzishwa mwaka 2015. Tamasha hilo linalofanyika Aprili kila mwaka, limekuwa likihusisha shughuli za kitamaduni kama vile maonesho ya vyakula vya kiasili, michezo na ngoma za utamaduni.

# Watanzania wachangamkia bidhaa za ndani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, amesema Watanzania wengi sasa wameanza kutumia bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini tofauti na awali

Beng'i alibainisha hayo juzi katika ziara ya siku moja mjini hapa wakati baraza hilo lilipomtembelea mjasiriamali Heri Mtanga katika mtaa wa Twendepamoja Kata ya Sofu, Halmashauri ya Mji Kibaha

Alisema awali Watanzania walikuwa wakithamini zaidi bidhaa kutoka nje kuliko zinazozalishwa ndani lakini kutokana na ongezeko la viwanda nchini na ubora wa bidhaa, vimesababisha kubadili mtazamo .

Akizungumza katika karakana ya Mtanga inayotengeneza mashine mbalimbali za kusagia nafaka, matofali na kutotolesha vifaranga, alisema baraza hilo linathamini wajasiriamali wadogo na kushirikiana nao ili kuwainua na kuwa wafanyabiashara wakubwa.

Issa alimwahidi mjasiriamali huyo kupata mkopo wa zaidi ya Sh. milioni 327 anazohitaji kwa ajili ya kuendeleza shughuli zake.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Martine Ntemo, aliwasihi wajasiriamali kuzingatia majina ya lebo za biashara zao ambayo yatakuwa rafiki kwa wateja wao.

Meneja wa Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Pwani, Beatha Minga, alikiri shirika hilo kumtegemea zaidi mjasiriamali Matanga kwa mkoa huo kutokana na kazi anazozifanya.

Mtanga aliwataka wajasiriamali kuachana na mawazo tegemezi ambayo yanawakwamisha wengine kupiga hatua.

Aidha , alisema kwa sasa vibali vingi vinapatikana bila kuwapo kwa urasimu kwenye taasisi husika.

Alisema tangu kuanzisha karakana hiyo mwaka 2012 hadi sasa, ameunda mashine 45 ambazo wameziuza ndani na nje ya nchi na kwamba changamoto anayokabiliana nayo kwa sasa ni mtaji ambao NEEC imeahidi kumpatia.



Mkurugenzi wa Huduma za Biashara wa Wakala wa Vipimo (WMA), Deogratius Maneno (kulia), akikabidhi msaada wa kompyuta 16 zenye thamani ya Sh. milioni 32, kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Jangwani, Nyaiburi Bhoke, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# WMA yaisaidia Jangwani kompyuta

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo Tanzania (WMA), imetoa kompyuta 16 zenye thamani ya Sh. milioni 32 kwa Shule ya Sekondari ya Jangwani ya jijini Dar es Salaam.

Msaada huo ulikabidhiwa jana na Mkurugenzi wa Huduma za Biashara wa WMA, Deogratius Maneno, kwa Mkuu wa Shule hiyo, Nyaiburi Bhoke, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa msaada huo, Bhoke alisema umekuja wakati mwafaka kwa kuwa shule hiyo ina mahitaji makubwa ya kompyuta.

Shule hiyo, alisema ina wanafunzi 200 wanaosomea kompyuta kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne lakini zilizopo ni 22 tu, hivyo wana upungufu mkubwa.

"Kwa wastani ni kwamba wanafunzi watano wanatumia kompyuta moja, hivyo tunaishukuru WMA kwa msaada huu ambao umekuja wakati mzuri na tuna hakika utasaidia kupunguza tatizo lililopo," alisema.

Pia alisema kompyuta hizo zitasaidia kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule hiyo hasa wale wanaosoma somo hilo.

Maneno kwa upande wake alisema wameona umuhimu wa kusiadia shule hiyo kongwe ambayo ina wasichana watupu ili kusaidia kuinua ufaulu wao.

Alisema lengo ni kuwahamasisha wasichana hao wasome kwa bidii na mwishowe watakapomaliza elimu yao ya vyuo vikuu wawe na shauku ya kujiunga na WMA kufanya kazi.

Mwanafunzi wa kidato cha kwanza shuleni hapo, Leokadia Abeid, aliishukuru WMA kwa msaada huo ambao alisema utawapunguzia adha ya kutumia kompyuta moja wanafunzi wengi kwa kuwa zilizopo hazitoshi.

Alisema wanafunzi wakijifunza kwa kutumia kompyuta na teknolojia ya kisasa ni rahisi kuelewa mambo mengi na kufaulu masomo yao kisha kuja kuwa viongozi bora wa baadaye.

Najma Nizar wa kidato cha kwanza shuleni hapo, alisema utamhamasisha binafsi kusoma masomo ya teknolojia.

# Kilo milioni 35.5 za tumbaku zanunuliwa

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

JUMLA ya kilo milioni 35.5 za tumbaku zimenunuliwa na kampuni mbalimbali hapa nchini tangu msimu wa ununuzi uliopozinduliwa Juni, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jana na Mteuzi Mkuu kutoka Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Albert Challe, kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya wakati wa ziara ya kikazi mkoani Tabora.

Alisema kiasi hicho ni sehemu ya makisio ya jumla ya kilo milioni 57.7 ambazo zilitarajiwa kununuliwa na kampuni hizo kununua msimu huu.

Challe aliongeza kuwa tumbaku iliyonunuliwa imewezesha kupata kiasi cha Dola za Marekani milioni 50.3, na kwamba bei ya wastani ilikuwa ni Dola 1.41 kwa kilo.

Alisema kati ya kilo hizo, kilo milioni 34.8 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 49.3 zilitokana na tumbaku ya mvuke (VFC) na kilo 700,000 zenye thamani ya zaidi dola 900,000 ni tumbaku ya moshi (DFC).

Challe alisema kushuka kwa uzito kulisababishwa na mvua nyingi iliyonyesha na kusababisha mbolea kutokaa katika mimea, jambo ambalo limewaathiri wakulima na kusababisha baadhi yao kushindwa kulipa madeni.

Alisema kufuatia athari hizo, Kampuni ya ununuzi wa Tumbaku ya Japan (JTI) imeamua kuongeza bei ili kuwasaidia wakulima walioathiriwa na mvua hizo.

Kusaya alitoa wito kwa kampuni nyingine kuangalia uwezekano wa kuwasaidia wakulima walioathirika na mvua ili angalao waweze kupata kiasi cha fedha cha kuridhisha.

# Wachachamalia kuporwa kituo cha mabasi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

ABIRIA na watumiaji wengine wa kituo kikuu cha mabasi katika Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera, wamelalamikia kuporwa mali zao wakati wa usiku kutokana na kituo hicho kutokuwa na taa za umeme na uzio.

Wakitoa malalamiko yao kwa Mkuu wa mkoa huo, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliyewatembelea kwa lengo la kusikiliza changamoto zinazowakabili, baadhi ya watumiaji wa kituo hicho walisema magari yanayotoka mikoani mengine hufika usiku na kulazimika kushusha abiria gizani, na kuwa baadhi hulala katika jengo la abiria ambalo pia halina taa. Mmoja wa wapiga debe katika kituo hicho, Adam Kichwabuta, alisema kwa kuwa serikali imeshindwa kukamilisha kituo kipya cha mabasi katika eneo la Kyakailabwa, basi wawekewe taa za umeme ili kupunguza madhara yanayowakumba ikiwamo kuporwa na wakati mwingine kujeruhiwa na vibaka.

Mwenyekiti wa chama cha kutetea haki za abiria mkoani Kagera, Bashiru Samadu, alisema mbali na kituo hicho kutokuwa na taa pia hakina uzio hivyo vibaka huwavamia abiria usiku na kuwapora.

"Kuna magari yanaingia hapa stendi usiku kutoka mikoani, abiria wengine hawana pesa za kwenda kulala katika nyumba za wageni, lakini pia hawawezi kupata magari yanayokwenda wilayani... hawa hulazimika kulala katika jengo la abiria na kuporwa mali zao, tunaomba kujengewa uzio ili abiria wawe salama," alisema.

Aidha, Samadu aliiomba serikali kuhakikisha wapigadebe na wabeba mizigo wanakuwa na sare zenye namba ili ikitokea wakafanya uporaji abiria wawatambue haraka.

"Hapa sifahamu kuna tatizo gani, maana hii nadhani ni stendi pekee Tanzania ambayo imeshindikana wapigadebe na wabeba mizigo kutokuwa na sare, hili nalo linaongeza uharifu," alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Gaguti ameahidi ndani ya siku saba kituo hicho kitakuwa na taa za umeme ili kuimarisha ulinzi na usalama kwa watumiaji.

"Nimewasikia, ili usalama uimarike lazima kuwe na taa, hapa taa lazima zifungwe nitalisimamia hili zifungwe ndani ya siku saba zitafungwa tena zenye mwanga mkali, usiku patakuwa kama mchana," alisema.

Kuhusu uzio, alisema serikali italifanyia kazi hata kwa kuanza na uzio wa gharama kubwa, ili baadae fungu likipatikana ujengwe uzio imara.

"Haiwezekani watu wanaingilia popote na kutokea popote, lazima tujenge uzio hata kama tutaanza wa gharama ndogo, lakini watu wote tuhakikishe wanaingilia na kutokea sehemu moja, hii itapunguza vitendo vya uharifu," aliongeza.



Mteja akichagua mananasi katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. Nanasi moja linauzwa kati ya 1,500/- hadi 2,000/. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waiomba serikali isaidie kulipwa fidia

**Na Samson Chache,** TARIME

WAKAZI zaidi ya 200 wa kitongoji cha Nyamichele, Kijiji cha Nyakunguru, wilayani hapa, wameiomba serikali iwasaidie kulipwa fidia za mali zao yakiwamo mashamba.

Walidai kuwa Mgodi wa Barrick North Mara unaozunguka maeneo yao, ulifanya tathmini tangu mwaka 2013 hadi sasa bila mafanikio ya kulipwa fidia.

Wakitoa kilio katika mkutano wa kitongoji cha Nyamichele na Kijiji cha Nyakunguru, kata ya Kibasuka, chini ya Mwenyekiti wa kijiji hicho, Chacha Sasi, aliyekuwa diwani kata hiyo, Joyce Manyata, walisema kuwa wananchi wao waliofanyiwa tathmini na mgodi huo kwa ajili ya kulipwa fidia tangu mwaka 2013 hadi sasa, hawajalipwa.

Walidai maeneo yao waliokuwa wakilima mazao ya chakula, wengi walisitisha kufanya shughuli za kilimo na wenye nyumba zilizokumbwa na zoezi hilo la tathimini, nyumba zao zimebomoka kutokana na kutofanyiwa ukarabati.

"Wananchi wa Nyamichele na Nyakunguru tunaiomba serikali ya awamu ya tano ya kuwatetea wanyonge chini ya Rais John Magufuli kuhimiza Mgodi wa Barrick North Mara ili uweze kuwalipa fidia wananchi waliofanyiwa tathimini."

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri, alisema maeneo ya kitongoji cha Nyamichele, kijiji cha Nyakungu, wananchi walifanyiwa tathmini ili walipwe fidia kama maeneo mengine ambayo kwa sasa ulipaji unaendelea vijiji vinavyozunguka mgodi huo yakiwamo maeneo ya Matongo na Nyabichune.

Alisema tatizo lililopo katika maeneo yaliyofanyiwa tathmini, baadhi ya wananchi wamepanda mazao usiku na kutegesha miche ya kahawa, migomba, katani na miti ya matunda katika eneo moja kwa nia ya kuhesabiwa miche hiyo ili ilipwe, kitendo ambacho kinakwamisha zoezi hilo kwa wananchi kukosa uaminifu. Kadhalika, Msafiri alisema baadhi wamekuwa mawakala kwa kununua maeneo ya watu wengine kwa kutegesha wakati awali tathimini ikifanywa hawakuwapo.

"Tunaendelea kufanya uhakiki wa majina ya watu wanaostahili kulipwa fidia na kuondoa majina ya watu wasio na sifa waliojipenyeza kwa nia ya ovu ya kutaka kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu," alisema.

Aliwataka wananchi hao kuwa na subira kwa kuwa ulipaji fidia unaendelea hatua kwa hatua na sawa ulipaji huo uko katika vijiji vya Matongo na Nyabichune na baadaye kuendelea katika maeneo mengine.

## Chanzo ongezeko watoto wa mitaani chawekwa bayana

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ONGEZEKO la watoto wa mitaani hasa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilayani Kahama mkoani Shinyanga, linachangiwa na ugomvi wa baba na mama katika familia na kushindwa kutimiza majukumu yao.

Imeelezwa kuwa hali hiyo inasababisha watoto kukimbia nyumbani kwenda kutafuta maisha.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa chama cha ushirika cha kuweka na kukopa (Mkombozi Saccoss) Kata ya Majengo, Baraka Ally, alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kuhusiana na chama kinavyowasaidia vijana wapiga debe, mawakala wa mabasi na mama lishe kujikwamua kiuchumi ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani.

Alisema asilimia kubwa ya watoto wanaokamatwa maeneo ya kituo cha mabasi katika Kata ya Majengo ni wanafunzi kutoka Halmashauri za Msalala, Ushetu na Mwakitolyo Shinyanga Vijijini na wanapowahoji zaidi wanadai wananyanyaswa na walezi wao, na kwamba ndio sababu ya kutoroka nyumbani kwao.

Aidha, Ally alisema wapo wanaoletwa na matajiri kwa lengo la kuwatumikisha kazi za ndani na kwenye migahawa, na kuongeza kuwa wanapoona mtoto mdogo mwenye umri wa kwenda shule akifanya shughuli yoyote ndani ya kituo hicho, wanamrejesha kwa wazazi wake mara moja.

Katibu wa chama hicho, Michael Masanja, alisema, mpaka sasa chama hicho kina wachama zaidi ya 600 wengi ni wapiga debe, mama lishe na watu wenye ulemavu, na wamekuwa wakijikwamua kiuchumi kwa kukopeshana fedha zenye riba nafuu.

Masanja alisema, mwaka juzi walifanikiwa kutoa mikopo ya Sh. milioni 60 kwa wanachama waliokidhi masharti ya uombaji wa mkopo na kuongeza mikopo hiyo imekuwa ikitolewa kwa wanachama mwenye shughuli.

Pia alisema kuwa, wanatarajia kuwekeza kwenye kilimo chenye tija kwa kiasi cha fedha walichonacho ili baadae wasajili ushirika imara wa kununua mazao ya kibiashara na kuuza nchi jirani.

Nae Samweli Katikiro, mwanachama, alisema tangu mwaka 2013 chama kimemsaidia kujenga makazi ya kudumu na kuondokana na kupanga sambamba na kuwasomesha watoto wake .

# Barabara Rusahunga-Rusumo yawaliza madereva wa malori

**Na Mohab Dominick,** NGARA

MADEREVA wa magari ya mizigo kutoka mikoa mbalimbali nchini, wameiomba Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutembelea barabara kipande cha Rusahunga-Rusumo mkoani Kagera ili kujionea usumbufu na adha wanayoipata madereva kutokana na uharibifu mkubwa wa barabara.

Baadhi ya madereva hao, Tumaini Josia, Iddi Khalifa, Mohamed Abed, Julius Kweyunga na Kurwa Mohamedi wakiongea na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti jana, walimuomba Waziri wa wizara hiyo, Isack Kamwelwe, kufika kwenye eneo hilo kusikiliza kero ya madereva kisha kuzitatua na kunusuru magari yao kuendelea kuanguka na kuharibika.

Madereva hao walisema licha ya ukarabati mdogo unaoendelea, lakini hauleti tija kwa barabara hiyo kwani sehemu hizo ni korofi na zinahitaji ukarabati mkubwa, na kuongeza kuwa hali hiyo kwao ni tatizo kubwa ambalo linapelekea magari yao kuharibika na kuanguka mara kwa mara hivyo kupelekea baadhi ya wamiliki wa malori kuanza kuihama barabara hiyo na kuhamia barabara ya nchi jirani ya Kenya, lengo la kusafirisha mzingo yao.

"Tunaomba serikali itusaidie sisi madereva angalau tuweze kupita kwa urahisi, magari yanaharibika kila siku, tunashinda hapa na kulala na sijui hatima yetu itakuwa lini... naomba serikali isikie kilio chetu, barabara ya Nyamugombe haifai," alisema Mohamedi Abed, mmoja wa madereva hao.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe ilitembelea barabra hiyo ambayo ni muhimu kwa uchumi, lakini pia huunganisha Tanzania na nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kushuhudia uharibifu huo.

Hata hivyo, akitoa ufafanuzi kwa njia ya simu kuhusu hali ya miundombinu mibovu ya barabara kutoka Rusahunga hadi Rusumo, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Elias Kwandikwa, alisema atahakikisha anatembelea barabara hiyo ili kujionea hali halisi, huku akisema mkakati wa serikali ni kuikarabati kabla ya mvua za masika kuanza.

"Asilimia 14 za ajali zinaweza kusababishwa na ubovu wa miundombinu ya barabara, lakini ndani yake kuna vitu vingine kama alama za barabarani na uharibifu wa watu ambao wanaweza kung'oa alama za barabarani, kwa hiyo mchanganyiko wa haya yote pamoja na mambo mengine ndio hupelekea ajali za barabarani," alisema Kwandikwa na kuendelea:

"Kuna kilometa 93, na mkakati wa serikali ni kupajenga hapo na maeneo yote korofi nchi nzima na kuna fedha nyingi zimetolewa kwenye maeneo korofi kimsingi, barabara ni kama binadamu huwa zinaishi kuanzia siku ya kwanza tu... ukimaliza unaendelea kufanya matengenezo, mvua zikinyesha zinachangia kuharibu barabara, lakini pia hata watu wengine magari yanaharibika, wanamwaga oil barabarani."

Aliwahakikishia watumiaji wa barabara kuwa serikali imejipanga kurekebisha kipande cha Rusaunga- Rusumo, na kwamba atawatuma makandarasi wa tatu ili kuhakikisha hizo kilometa 93 zitakamilika ndani ya muda mfupi kabla ya mvua kuanza.

# Nanyumbu kupata ghala la korosho

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na uongozi wa Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara wamekubaliana kujenga ghala la kuhifadhi tani 5,000 za korosho wilayani humo kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (SCGS) na kwa kushirikiana na Masasi and Mtwara Cooperative Union (MAMCU).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dr es Salaam baada ya mazungumzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, Moses Machali, alisema ghala hilo litatatua tatizo la hifadhi korosho wilayani humo na kuwaondolea usumbufu wakulima.

Alisema mipango ya TADB ni kuleta mageuzi makubwa katika kilimo ili kwenda sambamba na sera ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

Malighafi ni moja ya vitu muhimu na mazao ndiyo malighafi muhimu za viwanda vyetu. Tutajitahidi iwezekanavyo kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo ili kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa pato la faifa, alisema Justine.

Korosho ni kati ya mazao manane yanayotambuliwa na serikali kuwa ni mazao ya asili ya biashara. Korosho sasa limefanywa kuwa zao la kimkakati katika kuinua pato la wakulima na kuendeleza ajenda ya taifa ya uchumi wa viwanda. Uzalishaji wa korosho umekuwa ukiongezeka kila mwaka kutoka tani 155,416 msimu wa kilimo wa 2015/16 hadi zaidi ya tani 350,000 msimu 2018/2019.

Machali aliipongeza benki hiyo kwa kuhakikisha zao la korosho linaongezwa thamani na kuwa miongoni mwa zao la kimkakati.

"Naishukuru TADB kwa mchango wake wa kuleta maendeleo chanya katika Wilaya ya Nanyumbu. Ghala la kuhifadhi korosho litaufanya uzalishaji uongezeke na baadhi ya gharama zitapungua hususani za usafirishaji," alisema . Mashali.

Machali amesema kwa msimu wilaya yao ina uwezo wa uzalisha korosho katika tani 19,000 na kwamba ukosefu wa ghala ulikua ni changamoto kubwa sana katika kilimo cha korosho wilayani humo.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Sarah Chiwamba, akipata chakula cha mchana na baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Kitogoro, alipotembelea shule hiyo juzi, akiwa katika ziara ya kikazi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wafugaji Chalinze wamuita Waziri Mpina

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

BAADHI ya wakazi wa Kijiji Cha Magulumatali Kata ya Talawanda Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani, wamemuomba Waziri wa Mifugo na Uvuvi kufika katika kijiji hicho kusikiliza kero zao ikiwamo josho na daktari wa kuwachanganyia dawa za kuogeshea mfugo..

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi kijijini hapo, walisema sehemu ambayo josho lipo kwa sasa ambalo lilijengwa zaidi ya miaka 40 iliyopita wameambiwa ni eneo la wakulima, hivyo hawawezi kuendelea kuogeshea mifugo.

Maria Lemamba, mmoja wa wakazi wa Magulumatali, alisema, wanamuomba Waziri wa wizara hiyo, Luhaga Mpina kufika na kusikiliza kero zao kama anavyofanya katika maeneo mengine.

Orijuwa Leboy na Ngiras Natori, walisema mbali na changamoto ya josho, pia wanaomba kupatiwa daktari atakayewasaidia kuchanganya dawa kwa ajili ya kuogeshea mifugo yao kwa kuwa ofisa Mifugo wa Kata amewagomea, hali iliyosababisha baadhi ya mifugo yao kufa.

Alisema wamekuwa wakimshirikisha ofisa huyo, lakini hawakupata ushirikiano, hivyo kulazimika kuchanganya wenyewe dawa kinyume cha utaratibu wa kitaalamu na kusababisha mifugo kufa wakati ikiogeshwa.

" Tunaomba Waziri Mpina atufikie na sisi asikilize kero zetu kama itashindikana hata Naibu Waziri, Abdallah Ulega, afike Magulumatali kama alivyoenda katika vijiji vya jirani tupate haki kama wengine, tupate msaada wa daktari wa kutuchanganyia ili kuokoa mifugo yetu," alisema.

Ofisa Mifugo wa Kata hiyo, Ernest Less, alisema anatambua kero hiyo, na kwamba ameshindwa kutoa ushirikiano kutokana na eneo la josho kuwa katika migogoro baada ya uongozi wa Kijiji kusitisha shughuli ya kuogeshea mifugo katika eneo hilo.

Alisema sababu nyingine ni kutokana na Ulega kuahidi kushughulikia kero hiyo na kwamba kukosekana kwa majibu hadi sasa imechangia kwenda kufanya shughuli zake kama inavyotakiwa katika josho hilo..

" Hivi Karibuni Naibu Waziri Ulega alizungumza na wafugaji katika eneo la Chamakweza ambapo alifikishiwa kero ya josho la Magulumatali na kuahidi kutolea majibu, hivyo siwezi kwenda kuchanganya dawa wakati majibu ya wafugaji kuendelea kuogesha mifugo yao hapo bado hayajatolewa pamoja na migogoro iliyopo kijiji hapo ya josho kutumika lakini na la kusubiri, tamko la Waziri limechangia kuwa na ushirikiano hafifu."

Mwenyekiti wa Chama Cha wafugaji Kanda ya Mashiriki, Leton Leboy, alisema kazi ya chama hicho ni kiunganishi wafugaji na Serikali na kwamba kero zilizoelezewa atazifuatilia kwa ngazi husika.




Ukurasa 13

Baada ya Uwanja wa Mkapa, vipi jina lenu Taifa Stars?



Ukurasa 12

## TMDA yashikia bango Uchumi Viwanda kwa wazalishaji dawa

BUFE
IJUMAA AGOSTI 14, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

KUTOKA VIWANJA NANENANE...

# Mbunifu mashine aliyetangazwa na Oxfam, Majaliwa 'amuokotesha dodo'

• Aagiza nembo yake, kazi imeshaanza...

**Na Renatha Msungu, aliyekuwa Bariadi**

SIKU ya kilele cha Maonyesho ya 28 ya Wakulima (Nanenane), haiwezi kusahaulika kwa mjasiriamali Daudi Magari, ambaye kampuni ya Oxfam ilimfanya aonekane na serikali kuchukua jukumu la kumtangaza na kumtambua, kazi zake zijulikane ndani na nje ya nchi.

Leo hii ameshakuwa bidhaa ya ubunifu kitaifa, inayofanyiwa kazi kutangaza matunda ya ubunifu wa Kitanzania.

Mwanzo wake ilikuwa kama bahati yake siku hiyo, kwani kabla ya kufunga maonyesho hayo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitembelea mabanda ya maonyesho na alipofika katika banda la Oxfam,' lililokuwa ndani ya Halmashauri ya Kishapu, alimkuta Magari.

Hapo alikuwa akionyesha mashine rahisi ya kuchakata katani, yenye uwezo wa kuchakata kuanzia tani 40 kwa siku, jambo ambalo kiongozi huyo mkuu wa utendaji kiserikali aliliona kuwa ni maendeleo makubwa kwa mjasiriamali huyo.

Baada ya Waziri Mkuu Majaliwa kupata maelezo kuhusu mashine hiyo, aliagiza mjasiriamali huyo atambulike kwa taasisi zinazohusika na masuala ya mashine, ili ziwekwe kwa nembo yake binfasi na si vinginevyo.

Hapo Majaliwa alielekeza Wizara ya Viwanda na Biashara, kuanza kumfuatilia mjasiriamali huyo na kutoa maagizo kwa taasisi kama TEMDO,TILDO na SIDO, kushirikiana naye kutumia ubinfu wake, kutengeza mashine za kuchakata katani.

Ni matunda kutoka jitihda za wadhamini wa Oxfam, katika kuhudhuria maonyesho ya Nanenane, kama anavyoeleza Mratibu wa Fedha, Cecelia Makota, kwamba waliona kazi ya mbunifu magari ina mashiko, ndipo wakampeleka katika maonyesho ya Nanenane, wakiamini kazi yake ingeonekane.

Anasema, Oxfam ipo kwa ajili ya kuwainua wajasiriamali wabunifu, wanaokosa njia ya kutokea, wao wanawaibua kwa staili ya maonyesho. Makota anaendelea: "Tumefanya kazi kubwa Oxfam ya kuhakikisha Magari anaonekana, ndio maana serikali imepita na kutoa maagizo dhidi yake na yametekelezwa. "

Makota anasema, jukumu lao ni kuwainua wajasiriamali wabunifu wanaofanya kazi nzurina wanahitaji kutambulika kitaifa na kimataifa na anawaaalika wajasiriamali wengine kazi za kiubunifu, wasisite kuzifikisha Oxfam, ili nao wazitangaze.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Injinia Stella Manyanya, akiwa na Katibu Mkuu wake, Profesa Riziki Shemdoe, wakimsikiliza mbunifu wa mashine ya kuchakata katani, Daudi Magari. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

**WIZARA BIASHARA & VIWANDA**

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Injinia Stella Manyanya, anasema mbinifu Magari, amefika sehemu sahihi katika ngazi na safari ya ubunifu wake.

"Nawapongeza Oxfam, lakini nampongeza pia Magari kwa kazi yake ambayo imeonekana na serikali tumeitambua, "anasema Injinia Manyanya.

Anasema, wizara yake imekuwa ikikutana na wabunifu wengi na kuwatambua, hivyo kwa Magari, kutoka Kishapu,. Shinyanga.na Wizara ya Viwanda na Biashara imetekeleza agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, la kumuendeleza mbunifu Daudi, kufikia kuwa na mashine ya kuchakata mkonge inayotambulika kitaifa na kimataifa.

Kwa mujibu wa Naibu Wazairi, mbunifu huyo ataunganishwa na taasisi zinazohusika na uundaji mashine kama hizo, ili waungane naye katika uzalishaji wake.

"Huyu ni lulu kwa taifa na kuna wabunifu wengine wengi ambao hawajaibuliwa, naomba Oxfam watafuteni ili tupate wabunifu mbalimbali, "anasisitiza Injinia Manyanya.

Anaeleza lengo lililopo sasa, ni kuinua ubunifu wa kijasiriamali utambulike serikalini, ili wahusika wapige hatua na kufika mbali zaidi.

Ni katika hatua hiyo, Injinia anamuagiza Katibu Mkuu wa Wizara, Profesa Riziki Shemdoe, ahakikishe mashine inakuwa na jina la mbunifu, Daudi Magari, ambaye

naye analipokea kwa kuagiza (wiki mbili na nusu kutoka leo), wakurugenzi wa TEMDO, SIDO na TILDO wakutane na mbunifu wa mashine hiyo.

"Natoa hadi Agosti 30 kuhakikisha taasisi hizo zikutane na mbunifu huyo kwa ajili ya kumuinua na kutangaza kazi zake," anasema Profesa Shemdoe.

**MBUNIFU JE?**

Magari anaelekeza shukrani za kipekee kwa Oxfam, waliyoiona kazi yake na kuamua kumpeleka katika maonyesho ya Nanenane, akatangaze mashine hiyo.

Anasema amekuwa akizifanya vizuri kazi hizo za kibunifu, isipokuwa vikwazo vyake ni upatikanaji vifaa vya kukamilisha kazi zake, akiamini pindi zinapopatikana kazi za uzalishaji inakuwa nyepesi, hasa katika mashine hizo za kuchakataka katani

. Pia, anakiri kuwapo wabunifu wa kiufundi wengi wa aina yake wanaokwama kwa kukosa fursa za kujitangaza, hivyo katika Maonyesho ya Nanenane, serikali imekuwa ikitumia kuangalia ubunifu za wajasiriamali na kuzitambua kazi zao, ili ziwanufaishe.

UCHUMI

# TMDA yashikia bango Uchumi Viwanda kwa wazalishaji dawa

- Orodha ndefu ya wajenzi iko mezani
- Vitakasa mikono, barakoa viko sokoni

**Na Mary Geofrey**

AJENDA ya kukuza Uchumi wa Viwanda nchini inazidi kushika kasi baada ya wataalamu wa afya, kuja na yao kutilia mkazo uanzishwaji viwanda vya kuzalisha dawa kitaifa, ili kuendana na mipango ya nchi kujenga uchumi jamii ya watu wenye kipato cha kati.

Hiyo inafanyika huku kasi ya uwekezaji katika viwanda mbalimbali inaendelea kuongezeka, kutokana na idadi kubwa ya viwanda vinavvyofunguliwa, vikubwa na vidogo.

Ni mtazamo unaoshika nafasi, huku takribani asilimia 70 ya dawa zinazotumika nchini zinazalishwa nje ya nchi. Bado inatajwa kuwa kiwango kidogo sana cha uzalishaji wa dawa nchini.

Sasa hatua iliyoko ni kuwepo dhamira mahsusi ya kiserikali kuhakikisha inatimiza azma ya kuwapo viwanda vinavyojitosheleza kwa bidhaa za dawa nchini.

Hapo kuna azma mahsusi ya kuhakikisha kunatengezwa miundombinu rafiki, ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kupanua wigo wa ongezeko la viwanda nchini na katika eneo tajwa, kuna jicho la kipekee la kujengwa viwanda vya dawa.

Ni miaka mitano sasa, serikali nchini ya Rais Dk. John Magufuli nchi imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuanzisha viwanda vya dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Viwanda ni ajenda ya uongozi wa Rais Dk. Magufuli kwa lengo la kuifanya nchi kujitegemea yenyewe katika kuzalisha bidhaa zitokanazo na malighafi ya ndani na kuwezesha soko isijazwe na bidhaa kutoka nje ya nchi.



Meneja Udhibiti Ubora wa Kiwanda cha Viuadudu, Samwel Mziray (aliyegeuza mgongo), akifafanua jambo kwa washiriki wa Maonyesho ya Wiki ya Viwanda ya SADC, kuhusu matumizi ya dawa ya kuua mbu, walipofanya ziara kiwandani hapo, mwaka jana. Picha kulia ni sehemu ya kiwanda hicho.



### AJENDA YA TMDA

Katika kuunga mkono juhudi hizo, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imetekeleza kwa vitendo agizo hilo kwa kushirikiana na wawekezaji kujenga viwanda vya dawa na vifaa tiba 30.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, anasema viwanda vinavyozalisha dawa na vifaa tiba kwa sasa idadi yao inafika 14 nchini, katika mchanganuo wake, inajumuisha viwanda viwili vya kutengeneza dawa za binadamu na vya mifugo na vifaa tiba viko vitano.

Anasema, serikali imeweka msukumo mkubwa katika uanzishwaji viwanda hivyo, vikiwamo vya kutengeneza dawa za binadamu, mifugo na vifaa tiba.

"Wawekezaji 16 wapya waliwasilisha maombi ya usajili wa viwanda vipya vya dawa na vifaa tiba, ambavyo kwa sasa vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi," anasema Fimbo.

Anataja bidhaa zinazotarajiwa kuzalishwa, vinalenga kuzalisha dawa mbalimbali kama sindano aina za 'Sterile Small Volume Parenteral (SVP); Large Volume Parenteral (LVP); dawa za macho; na dawa za kupaka (Topical preparations); dawa za vidonge na maji (General Oral Solid Dosage forms & oral liquids); na dawa za chanjo ya mifugo.

Pia, anafafanua kuwapo viwanda vingine vilivyoanzishwa na kusajiliwa na TMDA, vinavyotengeneza barakoa (masks), vikubwa vipo vinne, vidogo na kati 66, hali kadhalika kuna viwanda 73 nchini, mahsusi kwa kutengenezaji vitakasa mikono.



Kiwanda cha kuzalisha dawa za binadamu kilichoko Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### USHAURI TMDA

Fimbo anasema, jitihada za TMDA kuhakikisha viwanda vinakidhi viwango muhimu, ni pamoja na kupitia pamoja na wamiliki kuhusu michoro tarajiwa ya viwanda na kuwashauri marekebisho, kwa kuzingatia matakwa ya kutaalamu, kabla ya ujenzi kuanza.

Lingine analonena, ni ushauri wa kitaalam kuhusu mashine na vifaa vinavyofaa katika uzalishaji na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa viwanda ili kuwaongezea uwezo .

"Tunakuwa tunaendelea kutoa ushauri na kufanya ukaguzi kwa viwanda husika vinavyoanzishwa,"anasema Fimbo na kufafanua kuwa, wanapunguza gharama za kusajili dawa za viwanda vya ndani, kutoka Sh. milioni moja na muda wa usajili kutoka miezi sita hadi miezi miwili.

Fimbo anawashauri wawekezaji waendelee kujitokeza kwa wingi kwa lengo la uwekazaji madhubuti ya viwanda vya dawa na hakuna tozo za ukaguzi wa viwanda na kuingiza malighafi, vifungashio na vifaa vya ujenzi

Anasema, TMDA imeanzisha madawati maalum ya kushughulikia viwanda vya ndani katika ofisi ndogo ya Dar es Salaam na Tume ya Taifa ya Uwekezaji (TIC), ikiwamo kuandaa vipeperushi vinavyoelezea utaratibu wa uanzishwaji viwanda.

Fimbo anaahisi mamlaka hiyo itaendelea kutekeleza azma ya serikali kuhamasisha na kusimamia uanzishwaji viwanda na kuviboresha vidogo vilivyopo, ili kufanikisha Sera ya Viwanda na sekta ya dawa nchini, lengo ni kuwezesha upatikanaji dawa bora, salama na zenye ufanisi kitaifa.

Kwa Upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Dawa na Vifaa tiba ,Akida Khea, anasema wawekezaji wa ndani wamepata mwamko mkubwa katika kuziba ombwe la uagizaji dawa nchini.

"Kati ya wawekezaji 16 waliokuja kuomba kujenga viwanda vya dawa na vifaa tiba, ambaye si Mtanzania ni mmoja tu, inamaana wawekezaji 15 ni Watanzania, hii itatusaidia kukuza kipato cha nchi na kuongeza ajira," anasema Khea.

Anaeleza kuwa, wamehakikisha wanafuata taratibu zote za uanzishaji viwanda vya namna hiyo.

"Tumekuwa tukiwatembelea mara kwa mara ili kuhakikisha hawakiuki sheria kwa kuwa haya ni maisha ya watu tutambue dawa ni sumu ukiitumia vibaya inakudhuru,"anasema Khea.

### TANZANIA VIWANDA

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amekuwa akitamka mara kadhaa, kwamba ili Tanzania kufikia lengo la Uchumi wa Viwanda, haina budi kuhakikisha kutimiza vigezo kadhaa, kikiwamo cha ukuaji uchumi kwa kiwango asilimia 12 kwa mwaka.

Anataja vigezo ni mchango wa viwanda katika Pato la Taifa usiopungua asilimia 15, utoaji ajira rasmi na za moja kwa moja uongezeke na kufikia asilimia 40 ya ajira zote na sekta ya viwanda iweze kuiingizia nchi mapato ya fedha za kigeni zaidi ya asilimia 25ya mapato yote ya fedha za kigeni.

"Viwanda ndivyo vimekuwa chimbuko la maendeleo ya haraka ya nchi mbalimbali duniani na mhimili mkuu wa kutegemewa katika kuondoa umasikini kwa kutoa ajira nyingi na za uhakika kwa wananchi. Maendeleo ya sayasi na teknolojia yanategemea sana sekta ya viwanda," anasema Majaliwa.

Anasema takwimu zinaonyesha katika mwaka 2018, sekta ya viwanda imetoa ajira rasmi 306,180 ikilinganishwa na ajira 280,899 za mwaka 2017; sawa na ongezeko la asilimia 9.


Moja ya viwanda vinavyohamasishwa ni vile vinavyochochea uzalishaji wa ajira kwa wingi.

Anasema ujenzi wa viwanda vipya nchini, katika kipindi cha Serikali ya awamu ya tano, umechangia kupatikana kwa ajira mpya 482,601 nchi nzima.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Baada ya Uwanja wa Mkapa, vipi jina lenu Taifa Stars?






NA JOSEPH KULANGWA

DUNIA imeumbwa ili kukaliwa na watu mbalimbali wenye mitazamo na maono tofauti. Wapo wanaojipenda na kujipendelea, lakini wapo wasioamini hivyo, ambao hufanya mambo na kusahau, wasijali kutambuliwa au kusifiwa.

Akimsifia Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, kwenye mazishi yake kijijini Lupaso, Masasi, Mtwara hivi karibuni, Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete alisema: "Alikuwa kiongozi thabiti, hakujali kusifiwa, maana unaweza kusifiwa ili uharibu."

Miongoni mwa mambo makubwa na ya kujivunia aliyofanya Mkapa katika uongozi wake, ni kujenga uwanja mkubwa wa michezo wenye uwezo wa kukaliwa na watu 60,000 kwa wakati mmoja, ambao ulikuwa ukijulikana kama Uwanja wa Taifa.

Ulipoteza jina hilo Julai 28, baada ya Rais Dk John Magufuli kukubali mapendekezo ya wadau, kuwa uwanja huo sasa uitwe jina la aliyeujenga, yaani Mkapa.

"Ingawa yeye hakuwa anapenda uitwe kwa jina lake, lakini kwa kuwa sasa hawezi kuniadhibu kwa kuwa amelala hapo, sasa natangaza kuwa utaitwa Mkapa…" alitamka Rais kwenye uwanja wa Uhuru siku ya mazishi ya kitaifa kwa Mkapa.

Vigelegele na makofi vilivyosikika, vilidhihirisha kuungwa mkono kwa tamko hilo la mkuu wa nchi, pia ni wazi wengi walikubali kumuenzi Rais huyo wa awamu ya tatu, kwa mchango wake huo adhimu katika tasnia ya michezo nchini.

Hata hivyo, bila shaka ni udhaifu tulio nao Watanzania, hasa viongozi tunaopewa dhamana ya kusimamia mambo mbalimbali, wa kusubiri kila kitu aseme Rais ndipo kifanyike. Hivi kweli wizara kuna siku ilithubutu kumwambia Mkapa au iliamua kuuita jina hilo ikakataliwa?

Je, ni lazima kusubiri mtu aage dunia ndipo awekewe kumbukumbu? Bila shaka si lazima, hivyo uwanja huu ulitakiwa uitwe rasmi Mkapa miaka mingi tu iliyopita, kama lilivyokuwa Daraja la Mkapa katika Mto Rufiji, shule na majengo mbalimbali yaendayo kwa jina lake.

Kwa kuwa Mkapa hakutaka kusifiwa, pengine ndiyo sababu alikaa kimya kwani alitenda wema akaenda zake, lakini pengine ndiyo sababu Rais Magufuli akasema hakutaka makubwa, hakupenda majina yake zipewe taasisi au miundombinu. Wachapa kazi mara nyingi hawaamini katika kusifiwa.

Napongeza uamuzi wa kuwa na uwanja mkubwa wa michezo unaoitwa Mkapa, utasaidia kuweka historia kwa vizazi vijavyo, ambavyo pengine havitakuwa vinamjua kwa kumwona au kumsoma, lakini angalau kwa kuona alichokiacha.

Kwa muktadha huo huo, bado nadhani Wizara inayohusika na michezo, ina deni la kuitafutia timu ya Taifa ya soka ya Tanzania jina. Hivi sasa inaitwa Taifa Stars (Nyota wa Taifa). Hilo si jina mahsusi la timu. Nchi zote zina 'taifa stars' wao.

Mathalan Kenya, wa kwao wanaitwa Harambee Stars, Uganda wana The Cranes, Zambia wana Chipolopolo, Afrika Kusini wana BafanaBafana na BanyanaBanyana (Wanawake), Rwanda wana Amavubi, Nigeria wana The Super Eagles, nk.

Kama timu ya Tanzania ya wanawake inaitwa Twiga Stars, kama timu ya wavulana inaitwa Serengeti Boys au Ngorongoro Heroes, kwa ni timu ya taifa ikose jina? Ikumbukwe hawa Serengeti, Ngorongoro na Twiga wote ni 'stars', wote ni nyota, lakini ili kuwatofautisha wana majina mahsusi.

Kana kwamba haitoshi, kwanini Shirikisho la Vyama vya Soka Tanzania (TFF) halijabuni nembo ya Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania kama zilivyo nchi zingine? Ligi Kuu ya Uingereza mathalan, ina nembo yenye kichwa cha mnyama simba, yetu Tanzania ni ipi? Badala yake tunatumia jina la mfadhili Vodacom kama nembo! Nani anakataza kuwa na nembo hiyo, mfadhili? Hapana. Kwa nini hatuna?

Ni vema Wizara husika ikafumbua macho na kuona umuhimu wa kuwa na jina la Timu ya Taifa ya Wanaume na nembo ya Ligi Kuu ya Soka, huku pia ikifikiria kuwa na Kombe la Ligi Kuu, lenye sura na umbile moja kama lilivyo la Dunia, la Afrika na hata la Azam. Alamsiki!

**• Simu: (+255) 713 410008 na baruapepe: jkulangwa@yahoo.com**

UCHUMI

# UCHUMI MAJI UNAPOGEUKA AJENDA RASMI KUTETEA RASILIMALI UMMA

- Mtazamo mkuu; matumizi, mtaji na nyenzo
- Tunaendaje? Elimu, umakini, vyanzo sahihi



Tukio la uzinduzi wa huduma ya maji. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Sabato Kasika**

DIRA ya Taifa ya Mwaka 2025, inalenga kuinua hali ya maisha ya wananchi, kwa serikali kufikisha kiwango cha juu upatikanaji maji kufikia vijijini na mijini.

Lengo lililopo serikalini sasa ni kuhakikisha inaendelea kuimarisha uwezo wa kusimamia rasilimali ya maji, ikiwa sehemu ya Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini awamu ya Pili (MKUKUTA -2).

Mkakati huo ulioanzishwa katika awamu ya pili ya uongozi wa nchi, unaozingatia kuongezeka kiwango cha upatikanaji maji, kama moja ya vipaumbele muhimu katika ajenda yake, kwa kuwa nchi ina mito mingi ya msimu inayotiririsha maji kipindi chote cha mwaka.

Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, anaitaja mito mikubwa ni pamoja na Ruvuma, Rufiji, Kilombero, Pangani, Wami na Ruvu, Malagarasi, Ruhuhu, Kiwira, Kagera, Bubu, Simiyu na Mara.

Anasema, katika kipindi cha Oktoba, mwaka jana na Februari, mwaka huu, mito hiyo imekuwa na maji mengi juu ya wastani wake.

**MAHITAJI YALIVYO**

Profesa Mbarawa anasema, mahitaji ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile nyumbani, umwagiliaji, viwanda na mazingira, ni wastani wa mita za ujazo bilioni 40 kwa mwaka.

Anafafanua:"Inakadiriwa mahitaji hayo ya maji yataongezeka hadi kufikia wastani wa mita za ujazo bilioni 57 kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

"Hii inaonyesha nchi yetu itaendelea kuwa na rasilimali za maji za kutosha, kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii."

Pia, anabainisha kwamba kutokana na mwenendo wa kuongezeka mahitaji ya maji nchini, ni muhimu nchi ikaendelea kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za maji na taifa lisiingie kwenye uhaba siku za usoni.

"Kwa mujibu wa 'Atlas' ya Taifa ya rasilimali za maji, toleo la mwaka 2019, nchi yetu inakadiriwa kuwa na rasilimali za maji zinazofaa kwa matumizi ya binadamu kwa wastani wa mita za ujazo bilioni 126," anasema.

Katika hizo anasema, pia zimo pia mita za ujazo bilioni 105 juu ya ardhi na za ujazo bilioni 21 ardhini na kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu milioni 54 nchini mwaka 2018, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa mita za ujazo 2,300.

"Kiasi hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa. Chini ya hicho, nchi huhesabika kuwa na uhaba wa maji," anasema.

**MALALAMIKO**

Ofisa Programu Mwandamizi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Deogratius Temba, anataja sababu zinazochangia kuwapo ukosefu wa maji, katika baadhi ya maeneo.

Temba anataja sababu mojawapo ni ukosefu wa elimu kwa jamii, inayowezesha kutambua umuhimu wa kulinda na kutunza vyanzo na miundombinu ya maji.

Pia, suala la kuhifadhi mazingira, vyanzo na miundombinu ya maji ni muhimu, ili kuhakikisha uendelevu wa huduma hiyo kwa jamii, hivyo suala la utoaji elimu kwa jamii haikwepeki.

"Sisi kama wadau wa maji na watetezi wa haki za wanawake, tunajua changamoto nyingi katika sekta hii. Unakuta kuna uharibifu wa miundombinu hiyo, unaofanywa na watu kutokana na ukosefu wa elimu," anasema Temba.

Anasema kuna wanaoendesha shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji na kusababisha huduma hiyo muhimu kukosa uhakika kwenye baadhi ya maeneo.

Kwa mujibu wa Temba, wizara inafanya jitihada mbalimbali ikiwamo kubainisha vyanzo vya maji na kuvihifadhi na kuunda Jumuiya za Watumia Maji, ikiwashirikisha wananchi katika mipango ya matumizi ya maji katika kidakio husika.

"Hatua hiyo ni nzuri, lakini jambo lingine ambalo linatakiwa kufanyika ni kuelimisha umma kutambua umuhimu wa kulinda na kutunza vyanzo vya maji ikiwamo pia ulinzi wa miundomboni ya maji kwenye maeneo yao," anasema.

Temba anaeleza kwamba, kuna watu ambao wakiona bomba la maji limepasuka kwenye maeneo lao, hata hawathubutu kutoa taarifa kwa mamlaka husika, badala yake inakuwa sherehe ya kupata maji ya bure, kwa kukinga kutoka sehemu iliyopasuka .

"Watu wa aina hiyo wanatakiwa kupewa elimu, watambue kuwa miundombibu ya maji inayowekwa kwenye maeneo yao, ni muhimu wailinde hata kwa kuweka vijana wa kufanya kazi hiyo ili idumu," anasema.

Temba anasema, elimu ikitolewa kwa umma, fedha zinazotarajiwa kutumiwa na Wizara ya Maji ambazo Sh.bilioni 733,284,075,000 katika bajeti ya mwaka 2020/2021, zitafanya kazi yake vizuri na kuzaa matunda katika enero hilo.

"Kila mmoja wetu ni mdau muhimu sana katika kusimamia ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji na miundombinu yake kwa ajili ya kuboresha huduma hiyo muhimu katika jamii," anasema.

> **"Sisi kama wadau wa maji na watetezi wa haki za wanawake, tunajua changamoto nyingi katika sekta hii. Unakuta kuna uharibifu wa miundombinu hiyo, unaofanywa na watu kutokana na ukosefu wa elimu," anasema Temba.**

**SERA ILIVYO**

Sera hiyo ya mwaka 1991, inalenga kuweka mfumo endelevu wa unaosimamia rasilimali maji nchini, unalenga kuandaa na kutekeleza taratibu za kisheria na kuweka muundo wa kitaasisi wenye uwezo wa kuitekeleza, ikiwamo kuwashirikisha kikamilifu walengwa wa huduma za maji.

Aidha, sera inalenga kutatua matatizo ya maji katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi, utunzaji na usimamizi endelevu wa rasilimali maji na ushirikishaji wa wadau wote katika kusimamia rasilimali za maji nchini.

Lingine, mtazamo unashikwa katika kuweka misingi endelevu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji, katika hali ya mabadiliko kiutendaji, hasa baada ya serikali kupunguza majukumu ya moja kwa moja kutoa huduma hizo na kubaki kuratibu, kushauri, kuwezesha, kusimamia na kutoa miongozo.





# Waziri aagiza mkandarasi umeme kukatwa bil. 4.76/-

**Na Paul Mabeja,** CHEMBA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameagiza kukatwa asilimia 10 ya malipo ya Kampuni ya A2Z Infra Engineering Limited, sawa na Sh. bilioni 4.76 kwa kuchelewesha kukamilisha mradi wa usambazaji umeme katika baadhi ya vijijii vya wilaya ya Chemba mkoani Dodoma.

Dk. Kalemani pia amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga, kushikilia hati za kusafiria za makandarasi husika na kuhakikisha hawatoki nje ya mkoa wa Dodoma, hadi watakapokamilisha kazi hiyo.

Waziri Kalemani alitoa maagizo hayo juzi wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya usambazaji umeme katika vijijini vya Farkwa na Banguma wilayani humo baada ya kuona kuwa mkandarasi huyo hajakamilisha kazi kama ilivyoainishwa kwenye mkataba. Alitakiwa kukamilisha na kukabidhi mradi Juni 30, mwaka huu.

"Hatuongezi fedha na miradi hii lazima ikamilike kwa wakati kwani mko nje ya muda huku wananchi wanahitaji huduma ya umeme na mkilipwa mtakatwa mishahara yenu," alisisitiza Dk. Kalemani.

Aidha, Dk. Kalemani alimtaka mkandarasi huyo kukamilisha kazi ya kuunganisha umeme katika vijiji vyote 66 vilivyobakia kabla ya Septemba 15 huku akisisitiza kuwa hakutakuwa na nyongeza ya muda wala msamaha.

Pia aliwataka makandarasi wote nchini wanaotekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini unaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuwa wamekamilisha usambazaji wa umeme ifikapo Septemba 15, mwaka huu.

"Maeneo yatakayokuwa yamebaki fanyeni ninyi (TANESCO) kukamilisha miradi hiyo ya usambazaji umeme na pesa iliyokuwa ilipwe kwa hao wakandarasi ilipwe kwenu", alielekeza Dk. Kalemani.

Vile vile, Dk. Kalemani alitoa siku 10, kufungwa transifoma katika kijiji cha Kwamtoro, Gonga, Babahi na Makorongo na Augosti 22, mwaka huu anakwenda kuwashia wananchi wa vijiji hivyo umeme.

Aidha, alimwagiza mkandarasi huyo kuongeza vibarua na magenge, ili kukamilisha kazi kwa wakati.

Hata hivyo Dk. Kalemani aliagiza Meneja wa TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) Mkoa wa Dodoma, kumweka pembeni msimamizi wa mradi wa REA mkoani hapa baada ya kushindwa kusimamia majukumu kikamilifu.

"Hatuwezi kufanya kazi kwa mazoea, hivyo mkandarasi atakayeshindwa kukamilisha na kukabidhi mradi wake Septemba 15, mwaka huu, na watendaji wote wa REA watachukuliwa hatua za kisheria kwani wananchi wanahitaji kupata huduma ya nishati ya umeme ninyi mnaleta mazoea kazini," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Odunga, alikiri kuwapo utendaji mbovu wa mkandarasi huyo kwa kutoonekana kazini kwa kipindi cha miezi sita.

"Mheshimiwa Waziri nakuhakikishia kuwa maelekezo yote uliyonipa nitayatekeleza kikamilifu na kwa wakati na kuhakikisha wananchi wetu wanapatiwa huduma stahiki", alisema Odunga.

Awali, akitoa taarifa yake kwa Waziri, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Frank Chambua, alisema kati ya vijiji 581 vya mkoa huo, vijiji 393 vimeshapata umeme ambavyo ni sawa na asilimia 67.47 ya vijiji vyote.



Waziri wa Nishati Dk. Medard Kalemani (wa tatu kulia), na Ujumbe wake, wakiwa katika ziara kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, wilayani Chemba, Mkoa wa Dodoma, juzi. **PICHA: WN**

# Sekta kilimo yakua asilimia tano

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SEKTA ya kilimo nchini imeelezwa kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.2, huku sekta ndogo ya mazao ikikua kwa asilimia 5.8 na kuchangia ongezeko la kasi ya ukuaji wa uchumi.

Hayo yalibainishwa jana na Kamishna wa Uendelezaji Sekta ya Fedha nchini, Charles Mwamaja, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, James Doto, katika ufunguzi wa warsha ya wadau wa ufuta inayofanyika jijini hapa.

Mwamaja alisema pato la taifa linalotokana na kilimo kwa kutumia bei za mwaka 2015, limeongezeka kwa asilimia 17 kutoka Sh. trilioni 25.2 mwaka 2015 hadi Sh. trion 29 kwa mwaka jana. Alisema hali hiyo inaonyesha sekta hiyo inavyoendelea kukua.

"Tunaona jinsi sekta hiyo inavyoleta mabadiliko kila mwaka, hivyo miaka mitano ya serikali imeonyesha jinsi gani inavyowekeza katika sekta hiyo ya kilimo," alisema Mwamaja.

Mwaka 2018 sekta ilichangia asilimia 28.2 ya pato la taifa huku sekta ndogo ya mazao ikichangia asilimia 16.2 na kwamba hali hiyo imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo vyakula vinavyotokana na mazao ya kilimo.

kati ya mwaka 2015 na 2019, sekta ya kilimo imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.2 ambapo sekta ndogo ya mazao imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.8.

"Kutokana na takwimu hizi, ni dhahiri kuwa uboreshaji wa sekta hii utaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa ujumla," alisema.

Alifafanua kuwa serikali imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha ahadi hii imetekelezeka ili wakulima waone faida katika kilimo ambacho wamekuwa wakifanya kila mwaka.

"Tunahitaji kuona wakulima wanafanya kilimo cha tija, ninyi ni mashahidi kwamba kwa sasa nchi inajivunia kuwa na Soko la Bidhaa mbalimbali," alisema Mwamaja.

Mwamaja alisema mfumo wa masoko wa sasa kama inavyofahamika hauko wazi kushindanisha nguvu ya soko bali uko mikononi mwa wanunuzi wachache ambapo bei inapatikana bila ushindani.

Alisema serikali kwa kutambua umuhimu wa mkulima na faida za Mfumo wa Stakabadhi za Ghala pamoja na mfumo wa mauzo kupitia Soko la bidhaa, Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT); Financial Sector Deepening Trust (FSDT).

Pia alisema Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imeandaa warsha hiyo ili kuwakutanisha Wadau muhimu wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa kwa mazao ya ufuta na korosho.

## Waonywa kupanga bidhaa barabarani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wafanyabiashara wanaopanga biashara kwenye barabara ya Nyerere Square kwa ajili ya soko la jioni, kuheshimu makubaliano na maelekezo yaliyotolewa.

Yuna aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao kwenye mkutano mkuu wao na kuwataka kuheshimu na kutii maelekezo yaliyoelekezwa kwao kwa ajili ya matumizi ya barabara hiyo.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara wanakiuka maelekezo ambayo yametolewa na halmashauri ya jiji, yanayowataka biashara zianzie kuuzwa muda wa jioni badala majira ya asubuhi.

Kwa mujibu wa Yune, barabara hiyo kwa muda wa asubuhi imetengwa ili itumike kupaki magari ambayo huliingizia jiji mapato.

"Kuna wamachinga hapa ambao ikifika majira ya asubuhi wanapanga biashara zao kwenye eneo hii la barabara bila kujali athari inayoweza kutokea ikiwamo ya kuzuia magari kupaki na kulikosesha jiji mapato ya ushuru wanaotozwa wakishapaki hapa," alisema. "Kutokana na dhana hii inaonyesha wazi kuwa baadhi yenu mnakaidi makubaliano yaliyowekwa baina yenu na halmashauri ya jiji na sisi kamwe hatutakubaliana na kitendo hicho cha kuzuia magari kupaki kwa sababu za biashara zenu," alisema.

Ofisa huyo alisema serikali kwa kushirikiana na halmashauri ya jiji, inawathamini wamachinga wote, hivyo kinachotakiwa ni kutii mamlaka husika ili wafanye biashara zao kwa uhuru bila kubughudhiwa.

Awali, wakizungumza katika mkutano huo, wafanyabiashara hao waliiomba halmashauri ya jiji kuruhusu siku za Jumamosi na Jumapili wafanye biashara zao kuanzia majira ya asubuhi ili kujiongezea kipato zaidi.





# Tulia Trust yatoa mifuko 140 saruji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TAASISI ya Tulia Trust inayojishughulisha na utoaji huduma mbalimbali kwa jamii ndani na nje ya mkoa wa Mbeya, imetoa msaada wa mifuko 140 ya saruji katika shule za msingi za Halinji na Nsalaga zilizopo jijini hapa.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo ambaye pia ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alikabidhi msaada huo jana na kusema lengo la kufanya hivyo ni kuwasaidia watoto kusoma kwa furaha.

Alisema msaada huo hauna uhusiano wowote na masuala ya siasa bali ni kutoa huduma za kijamii kwa wananchi kwa kuwaletea maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, shule na mikopo.

"Taasisi ya Tulia Trust imekuwa ikitoa msaada wa hali na mali kwa wakazi walioko ndani na nje ya mkoa kwa kuhakikisha inajenga na kuboresha huduma mbalimbali.

"Nawaomba wananchi suala hili na taasisi yangu lisihusishwe na mambo ya kisiasa kwa sababu muda wa kampeni bado na mimi hapa sijaja kama mgombea bali nimekuja kama kiongozi wa taasisi," alisema Dk. Tulia.

Katika hatua nyingine, Dk. Tulia alipokea madawati 200 kutoka kampuni ya bomba la mafuta inayofanywa kwa ubia wa nchi ya Tanzania na Zambia ya Tazama Pipeline.

Alisema madawati hayo yatagawanywa kwa shule mbalimbali za msingi na sekondari jijini Mbeya ambazo zina upungufu ili kusaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi na kusoma kwa utulivu.

# TGNP yajitosa rushwa kwenye uchaguzi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MTAALAM wa sosholojia na masuala ya ufuatiliaji na tathmini kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Gratiana Rwakibarila, ameiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na vyombo vingine vinavyohusika na masuala ya utoaji haki, kuhakikisha wagombea wote waliohusika na utoaji rushwa wanachukuliwa hatua.

Rwakibarila alisema hayo jana wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Mbeya na Ruvuma yaliyolenga kujenga na kuongeza uelewa na uwezo katika kuripoti masuala ya kijinsia na kuhamasisha ushiriki wa wanawake na vijana kwenye uongozi.

Alisema rushwa inachangia kwa kiasi kikubwa kupokonya haki za wananchi ambao wana sifa ya kuwa mahali fulani lakini kutokana na hilo, wengi hawatendewi haki.

Mtaalam huyo alisema moja ya mada ambazo zinaongelewa kwa sasa ni rushwa kwenye mchakato wa kura za maoni kwenye nafasi za udiwani na ubunge na kwamba wenye fedha walitoa ili kupata nafasi vile vile rushwa ya ngono.

"Tunaviomba vyombo vinavyohusika na utoaji haki, vihakikishe hakuna mgombea yeyote aliyehusika na rushwa hapewi nafasi ya kugombea nafasi yeyote ili kuwapa nafasi wale ambao walikuwa na sifa wagombee. Sisi TGNP tunaamini katika usawa na haki," alisema Rwakibarila.

Aidha, aliwashauri wanahabari kuwapa wanawake na vijana waishio vijijini (pembezoni) nafasi kwenye vyombo vyao ili waeleze malengo na shughuli watakazofanya endapo watapewa nafasi ya kugombea uongozi.

Vilevile alisema watu wenye ulemavu wafuatwe huko waliko ili kupewa nafasi ya kueleza waliyonayo katika kuwatumikia wananchi bila kujali aina ya ulemavu walionao.

"Waandishi wa Habari nchini nawaomba wafanye ulinganifu katika makundi yote hususani wanawake na vijana ambao walijitokeza kwenye kiny'ang'anyiro za uongozi kuanzia udiwani hadi ubunge kuwafuatilia ili kujua wanayofanya kuelekea uchaguzi mkuu. Hii itasaidia kutoa haki," alisema Rwakibarila.

Alisema hali hiyo itasaidia kuwapa moyo na kuwahasisha wanawake kufahamika kwa wapiga kura wao bila kujali maeneo yao wanakotoka.

Aliwahamasisha wagombea wote kutokubali kukatishwa tama na suala la rushwa badala yake wajikite kueleza sera na mikakati yao kuwatumikia wananchi endapo watapata ridhaa ya kuwaongoza.



Mtaalamu mwelekezi wa masuala ya upangaji bajeti ngazi ya familia kutoka Shirika la Elimisha la jijini Mbeya, Festo Sikagonamo, akizungumza kuhusu umuhimu wa upangaji wa bajeti kwa vijana wa Kata ya Igawilo, jijini humo, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanahabari watakiwa kupima afya

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya magonjwa ya mlipuko ikiwa ni pamoja na kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara.

Mtaalam wa maabara kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Cloudy Mgaya, aliyasema hayo juzi wakati wa mafunzo kwa wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MBPC).

Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwakumbusha kuchukua tahadhari katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwamo maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema wanahabari wanapaswa kujenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara ili kujiepusha na madhara yanayoweza kutokea endapo atabainika kuwa mgonjwa.


"Wanahabari mmekuwa mstari wa mbele kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na magonjwa mbalimbali ya mlipuko ikiwamo vita dhidi ya corona. Hakika mmefanya kazi kubwa lakini nawaomba nanyi mchukue tahadhari kwa kuzingatia kanuni zote za afya pamoja na kupima afya mara kwa mara," alisema Mgaya.

Aidha, Mgaya aliwaomba wanahabari wa Mkoa wa Mbeya kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya magonjwa ya mlipuko kwa kuwahamasisha kunawa mikono mara kwa mara, kuvaa barakoa na kuzingatia umbali wa kuanzia mita moja wakati wa kupata huduma sehemu zenye mikusanyiko.

Mwenyekiti wa MBPC, Festo Sikagonamo, alisema elimu waliyoipata juu ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko itawasaidia kuwa salama katika kutimiza majukumu yao ya kihabari.

Mwanachama wa chama hicho, Charles Mwakipesile, aliwaomba wanahabari kuelekea uchaguzi mkuu kuzingatia maadili ya uandishi ili kuepusha chuki na madhara kwa vyanzo vya habari na jamii kwa ujumla.

Alisema ni wakati sasa kwa wanahabari kuwa makini kuripoti habari za uchaguzi kwa kujiepusha na ukereketwa wa chama chochote cha siasa..



# Wizara kuleta mageuzi sekta ya kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, amesema kuwa wizara hiyo imelenga kuendeleza mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kuifanya ya kisasa, jumuishi na yenye ushindani.

Alisema kuwa sekta ya kilimo ikijumuisha mazao, mifugo, uvuvi, misitu na rasilimali zisizorejesheka bado inaendelea kuwa ni muhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar.

Alisema hayo Ikulu Mjini Zanzibar wakati akiwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mwaka 2019/2020 na wa mwaka 2020/2021.

Alisema sekta hiyo inatoa mchango wa moja kwa moja kwa wananchi katika kujikimu kimaisha na asilimia 40 wameajiriwa na sekta hiyo na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hiyo na kwa mwaka 2019 imechangia asilimia 21.2 ya Pato la Taifa. Akieleza kuhusu wizi na uchimbaji holela wa rasilimali ya mchanga, Waziri Mjawiri alisema kuwa wizara kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi vya Zanzibar, imeunda kikosi shirikishi cha doria ambacho kinaendelea kupambana na wizi na uchimbaji wa mchanga kiholela na udhibiti wa ukataji ovyo wa miti.

Alieleza Mpango Kazi wa mwaka 2020/2021 ambao umelenga kuleta Mapinduzi ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kutoka Kilimo duni cha kujikimu kuelekea kilimo endelevu cha kibiashara na chenye tija pamoja na uhifadhi na matumizi. Pia, jumla ya wafanyakazi 263 wameajiriwa ikiwamo wahudumu shambani, maofisa katika ngazi tafauti na wataalamu 68. Dhamira ya wizara hiyo ya kuibadilisha sekta ya kilimo kuwa ya kibiashara ni kwa kuhamasisha ukuaji wa viwanda vidogo, miradi ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, utumiaji wa teknolojia za kisasa, uzalishaji na usindikizaji wa mazao ya kilimo, kuongeza uzalishaji pamoja na kuweka mazingira bora katika sekta hiyo.

Alisema kuwa wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 inalengo la kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji katika eneo la hekta 65 na kukarabati hekta 87. Alisema pia inatarajia kuongeza uzalishaji wa mpunga kufikia wastani wa tani 50,000 na kuendelea kutoa huduma za matrekta na zana zake kwa wakulima na kufuatilia ukulima wa zao la mpunga katika eneo la ekari 33,800 na mazao mengine ya kilimo. Alisema wizara hiyo pia, itafanya utafiti wa kisayansi, kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa 'Zanzibar Research Agenda' kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi na kuimarisha miundombinu ya utafiti. Naye RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuendelea kufanyakazi kutokana na kupata mafanikio makubwa.

Dk. Shein alieleza imani yake kwamba zoezi hilo limesaidia kwa kiasi kikubwa kutathmini shughuli za wizara za serikali.

Alisema kuwa serikali imeweka mkazo kufanya utafiti hatua ambayo imesababisha kuanzisha taasisi mbalimbali na kituo cha utafiti cha Kizimbani ndio cha kwanza katika nchi za Afika Mashariki hali inayoonyesha kuwa Zanzibar imepiga hatua muda mrefu.

Alisema taasisi hizo zimeundwa kwa ajili ya kuendeleza kilimo, uvuvi na afya kwa lengo la kuleta tija na Zanzibar itakwenda mbele katika sekta ya kilimo kutokana na programu mbalimbali zinazotekelezwa na wizara hiyo.



Mkurugenzi Idara ya Elimu Sekondari, Asya Iddi Issa, akitoa maelezo kuhusu idara yake, katika kikao cha utekelezaji wa mpango kazi kwa kipindi cha Mwaka 2020/2021 cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kilichofanyika katika ukumbi wa Ikulu Mjini Zanzibar jana, chini ya Mwenyekiti wake, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani). **PICHA: IKULU**

# Naibu Msajili avipongeza vyama kwa uwazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Mohamed Ali Ahmed, amevipongeza vyama vya siasa kwa kufanya uchaguzi wao wa ndani na kuwapata viongozi katika hatua ya awali kwa uwazi na kufuata misingi ya demokrasia ikiwamo baadhi ya vyama kurusha matangazo mubashara.

Akizungumza na wandishi wa habari ofisini kwake Chukwani, alisema wameshuhudia hatua ya awali ya mchakato wa kupata viongozi wa vyama ukifanyika kwa njia ya kidemokrasia ambayo imewaridhisha wagombea na kuondoa malalamiko.

Alisema sheria ya msajili wa vyama vya siasa inavitaka vyama hivyo kuendesha shughuli zao kwa uwazi katika hatua mbalimbali ikiwamo kutafuta viongozi.

Alisema anaamini katika hatua nyingine inayofuata ya kufanya kampeni za kisiasa, viongozi wa vyama hivyo watazingatia maadili, na sheria ikiwamo kufanya kampeni za kistaarabu zenye kuzingatia na kulinda amani na utulivu. Alisema baadhi ya vyama vya siasa mchakato wake wa kupata wagombea nafasi ya urais ulikuwa wazi na kufahamika kwa kila mwanachama mwenye nia ya kugombea nafasi hiyo hadi katika hatua za mwisho ikiwamo za kupigiwa kura.

"Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa Zanzibar imeridhishwa na utendaji wa vyama vya siasa katika mchakato wa awali wa kupata viongozi watakaoshiriki katika hatua mbalimbali za uchaguzi mkuu na matarajio yetu makubwa uchaguzi mkuu ujao utafanyika kwa amani na utulivu," alisema. Alivitaka vyama vya siasa kuzingatia mafunzo waliyopatiwa na Ofisi ya Msajili ikiwamo kuimarisha amani na utulivu na kuzingatia usawa wa kijinsia katika kupata viongozi wa nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema sheria ya Msajili wa Vyama vya Siasa inavitaka vyama kuweka usawa wa kijinsia kwa nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali za juu kuanzia nafasi ya urais, uwakilishi, ubunge na udiwani na kuona kundi la wanawake linashirikishwa na hatimaye kuingia katika vyombo vya uamuzi vya kutunga sheria.

Alivipongeza baadhi ya vyama vya siasa nchini kwa kuonyesha mwelekeo mzuri wa kuzingatia usawa wa kijinsia ikiwamo kuwateua wanawake katika nafasi ya urais, ugombea mwenza pamoja na ubunge na uwakilishi.

"Tunavipongeza baadhi ya vyama vya siasa nchini vimezingatia matakwa ya sheria ya Msajili wa vyama vya siasa vya kutoa nafasi kwa wanawake kugombea nafasi za juu...vipo vyama vya siasa wameteua wagombea mwenza wanawake huku wabunge na wawakilishi wakipewa nafasi zaidi," alisema.

## Samia azitaka redio jamii kutoa elimu udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Rais wa Muungano, Samia Suluhu Hassan, amezitaka redio jamii nchini kutoa elimu zaidi kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambapo baadhi ya tafiti zinaonyesha watoto wa kiume kuathirika vibaya na matukio hayo.

Suluhu alisema hayo huko Binguni Wilaya ya Kati Unguja, wakati akifungua kituo cha redio jamii ambacho ujenzi wake umefadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Alisema matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa jamii ya watoto wa kiume hivi sasa yanasikitisha na kama hakuna juhudi za makusudi za kupambana na athari hizo ipo hatari ya taifa lijalo kizazi kukosa nguvu kazi na uwezo wa kuongoza nchini.

"Nimesikitishwa na taarifa za matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo vimeshika kasi kwa kundi la watoto wa kiume kuharibiwa...tusipochukua tahadhari ipo hatari ya kizazi kijacho kukosa nguvu kazi inayotegemewa," alisema.

Aliitaka jamii ya Wazanzibari kuacha 'muhali' na kutoa taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia kwa taasisi husika ikiwamo jeshi la polisi na kufanyiwa kazi.

Alisema bado wapo wanawake wanaoficha matukio hayo kwa kuwahifadhi waume zao ambao hufanya ukatili wa kutisha katika familia zao kwa kuogopa kupewa talaka.

"Zipo taarifa kwamba wanawake wanaogopa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili vinavyofanywa na waume wao katika familia eti kwa kuogopa kupewa talaka," alisema.

Naye Waziri wa Habari Utalii na mambo ya kale, Mahmoud Thabit Kombo, alilipongeza Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni kwa kusaidia kuendesha vituo vya redio jamii vilivyopo Zanzibar na kusaidia kufikisha ujumbe wa matukio mbalimbali kwa wananchi.

"Tunazo redio jamii nyingi Unguja na Pemba ambazo zimetusaidia kwa kiasi kikubwa kufikisha ujumbe na taarifa za matukio mbalimbali kwa ajili ya ustawi wa jamii na wananchi wetu," alisema.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Shirika la UNESCO nchini, Tirso Do Santos, aliwataka wasimamizi wa redio jamii kuzitumia kutoa elimu ya mambo mbalimbali ikiwamo suala zima la kudumisha amani na utulivu katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu.

"Tunakabiliwa na uchaguzi mkuu wa Oktoba na redio jamii zetu zinatakiwa kufikisha ujumbe wa viongozi na wananchi kudumisha amani na kuepuka vurugu za kisiasa ambazo athari zake ni kubwa," alisema.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



**Thadey A. Mauki** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1004-0061** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2002 katika shule ya Sekondari Mnini, Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0620-0893** iliyotolewa na Baraza la mithihani mwaka 2007 katika shule ya Sekondari Tegeta na cheti cha chuo chenye namba **E0501-0272** kilichotolewa na Butimba College mwaka 2011. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Polisi Taarifa: B/VOL.45**

## KUPOTELEWA KADI YA GARI

**FREDERICK M. LWEZAULA**
AMEPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA LANDCRUISER LENYE NAMBA ZA USAJILI **T993 AJM,** INJINI Na. **3F0207419** NA CHESIS Na. **FJ62098179.** AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA RB NAMBA **KAG/BUK/RB/31031/2020.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE AU APIGE SIMU NAMBA 0784-333551

115857802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MIKONGENI.**

**Usimamizi wa mirathi No;18/2020**

**Ombi la JOSEPH AUGUST SHAYO,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SILVIA HENRY NJUU.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/08/2020.

Sahihi ya Hakimu

115858002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO- MJINI**
**WILAYA YA DODOMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**SHAURI LA MADAI 283, 284, 285, 286, 287, na 288 YA 2020**

**MDAI................ WANTORA J. N. BUSINESS SOLUTION CO. LTD.**

**DHIDI YA**

**WADAIWA............ 1. RASHID HAMZA ISSA, 2. CHINGA SAMWEL CHILEMELA, 3. GERALD C. MWANILYELA, 4. CHRISTOPHER FREDRIC MAHENDE, 5. DANIEL FULKO HAULE, 6. BENJAMINI ANDREA NYANJUKU**

Kwa kuwa Mdai mtajwa hapo juu alifungua mashauri dhidi yenu wadaiwa watanjwa hapo juu.
Mnaamriwa na jamuhuri kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 24/08/2020 bila kukosa ili kuja kujibu madai hayo dhidi yenu.

Endapo hamtahudhuria mbele ya mahakama siku hiyo shauri/mashauri hayo yatasikilizwa upande mmoja ( Exparte Hearing) na kutolewa maamuzi.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na mahakama hii leo tarehe 10/08/2020.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI
DODOMA

115857702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO- MJINI**
**WILAYA YA DODOMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**SHAURI LA MADAI 338, 339, 340 na 341 ZA 2020**

**MDAI.................. WANTORA J. N. BUSINESS SOLUTION CO. LTD.**

**DHIDI YA**

**WADAIWA..................... 1. BENADETTHA THOMAS MAGESA, 2. JULIUS ANDREA JULIUS, 3. GODLUCIS DAMIAN PASKAL, 4. YUSUPH JAMES WANYABANGOYE.**

Kwa kuwa Mdai mtajwa hapo juu alifungua mashauri dhidi yenu wadaiwa watanjwa hapo juu.
Mnaamriwa na jamuhuri kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 28/08/2020 bila kukosa ili kuja kujibu madai hayo dhidi yenu.

Endapo hamtahudhuria mbele ya mahakama siku hiyo shauri/mashauri hayo yatasikilizwa upande mmoja ( Exparte Hearing) na kutolewa maamuzi.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na mahakama hii leo tarehe 11/08/2020.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI
DODOMA

115857702

---

**TANGAZO**

**FORM 11**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MARANGU**

**USIMAMIZI WA MIRTHI NO 23/2020**

**Ombi la INNOCENT ALFRED MOSHA**

**Msimamizi wa mirthi ya marehemu ALFRED MOSHA**

**YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**TANZANIA**
**BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka,mnamo tarehe 01/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa misimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 12/08/2020

SAHIHI YA HAKIMU

115857302

---

**TANGAZO**

**FORM 11**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MARANGU**

**USIMAMIZI WA MIRTHI NO 22/2020**

**Ombi la INNOCENT ALFRED MOSHA**

**Msimamizi wa mirthi ya marehemu JULIE ALFRED MOSHA**

**YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**TANZANIA**
**BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka,mnamo tarehe 01/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa misimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 12/08/2020

SAHIHI YA HAKIMU

115857302

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO.112/2020**

**DEBORA R. NYAMIZI.....................................................MDAI**

**DHIDI YA**

**EMANUEL JORAM KASEKWA.....................MDAIWA NO. 1**

**FINCA MICROFINANCE LTD.........................MDAIWA NO. 2**

**PETER MUHEZYA MBOYA.........................MDAIWA NO. 3**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: EMANUEL JORUM KASEKWA**

Fahamu kwamba shauri amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 27/08/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. T. Munzerere Mwenyekiti wa baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zitapatikana katika masijara ya baraza la ardhi na nyumba Mbeya.

Unaaumriwa kuudhuria mbele la baraz siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya.
**Kumbuka:** usipoudhuria siku hiyo baraz litatoa amri stahili ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 03/08/2020.

T.Munzerere
MWENYEKITI

115857502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo ya MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi 77 /2020.**

**Ombi la ISSA HAMISI SAIBU kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu HAMISI ATHUMANI NDWATA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 01/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Tarehe 11/8/2020

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
DODOMA

115857602


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mgombea wa urais FDC akataa kuwania mwakani

**KAMPAKA, Uganda**

CHAMA cha The Forum for Democratic Change (FDC) nchini Uganda, kipo njia panda baada ya muasisi wake na mgombea mara nne wa urais, Kizza Besigye, kukataa ombi la kupeperusha tena bendera ya chama hicho Uchaguzi Mkuu mwakani.

Dk. Besigye, ambaye alipambana mara nne na Rais Yoweri Museveni tangu mwaka 2001, kila mara alimshutumu Rais huyo kuiba kura.

Mwaka 2001 na 2006 alikwenda katika mahakama ya juu na katika kesi zote kwa kauli moja majaji walithibitisha kuwa kulikuwa na wizi wa kura lakini kwa mgawanyiko wa kura haukutosha kubatilisha matokeo ya mwisho ya kura.

Uamuzi wa Dk. Besigye wa kutogombea tena urais mwakani umekiacha chama chake kikimtafuta atakayekiwakilisha katika uchaguzi huo.

Tayari chama hicho kimeaihirisha mara mbili uteuzi wa wagombea wake wa urais kwa matumaini kuwa Dk. Besigye angebadili msimamo wake na kuchukua fomu za uteuzi.

Mwaka 2019 mbunge wa upinzani Uganda, Robert Kyagulanyi na mwanaharakati wa kisiasa na mpinzani Dk. Kizza Besigye waliahidi kushirikiana kukiondosha madarakani chama tawala National Resistance Movement (NRM) kinachoongozwa na Rais Museven.

Akizungumza na kituo cha televisheni cha NTV, Besigye alikataa kujibu swali kuhusu iwapo atagombea urais 2021 au la.

Mara nyingi alisisitiza kuwa swali hilo ni kosa na alisema hakuna uchaguzi utakaomng'oa madarakani Rais Museveni.

"Hatuhitaji uchaguzi ili tupate uhuru. Mkakati unaopaswa kutuandaa kupigana kwa ajili ya nchi yetu uchaguzi uwapo au bila uchaguzi," alisema.

Dk. Besigye ni mpiganaji wa zamani na daktari binafsi wa Museveni wakati wa vita vyao vya msituni vya kati ya mwaka 1981 hadi 1986 vilivyoweka madarakani vuguvugu la NRM.

Safari ya Dk. Besigye ya kutaka kuwania kiti cha urais nchini humo haikuwa rahisi, mara kwa mara alitaka kufungwa na hata kupigwa na maofisa wa usalama hususani alipojaribu kutafuta haki hiyo.

***BBC***




Mgombea mara nne wa urais kupitia chama cha The Forum for Democratic Change (FDC) nchini Uganda, Kanali Dk. Kizza Besigye, akiwa mikononi mwa polisi katika moja ya matukio ya kukamatwa mara kwa mara na polisi wakati wa uchaguzi.**PICHA:MTANDAO**

## Mahasimu kisiasa wajitosa kumshambulia Trump

**WASHINGTON, Marekani**

MGOMBEA wa urais nchini Marekani kupitia chama cha Democratic, Joe Biden, pamoja na mgombea mwenza wake, Kamala Harris waweka kando uhasama wao wa awali wa kisiasa na kumshambulia Rais Donald Trump.

Wawili hao walijitokeza kwa pamoja mara ya kwanza juzi na corona iliwazuia kuwahutubia wafuasi wao katika ukumbi uliojaa na badala yake walitoa hotuba yao katika ukumbi uliokuwa na waandishi wa habari na familia zao tu.

Harris ndiye aliyeonekana kumshambulia Trump zaidi kuhusiana na namna alivyolishughulikia janga la virusi vya corona Marekani.

"Virusi hivi vimeathiri nchi zote ila kuna sababu iliyoifanya Marekani kuathirika zaidi ya mataifa yote yaliyoendelea, ni kwa sababu ya Trump kushindwa kulichukulia suala hili kwa umuhimu kutoka mwanzo. "Lakini, tuwe wazi kwamba lengo la uchaguzi huu siyo kumshinda Trump na Mike Pence tu, lengo ni kuijenga nchi hii iwe bora tena."

Kuchaguliwa kwa Harris katika nafasi ya mgombea mwenza wa Biden kumeleta siyo tu uzito wa kihistoria katika kampeni hiyo, bali pia ni jambo lililoiinua kampeni yake katika suala la uchangishaji fedha za kampeni.

**DW**

**"Virusi hivi vimeathiri nchi zote ila kuna sababu iliyoifanya Marekani kuathirika zaidi ya mataifa yote yaliyoendelea, ni kwa sababu ya Trump kushindwa kulichukulia suala hili kwa umuhimu kutoka mwanzo. "Lakini, tuwe wazi kwamba lengo la uchaguzi huu siyo kumshinda Trump na Mike Pence tu, lengo ni kuijenga nchi hii iwe bora tena."**

## Ujerumani ina matumaini chanzo corona

**BERLIN, Ujerumani**

WAZIRI wa Afya wa Ujerumani, Jens Spahn, amesema kuwa ana matumaini ya kupatikana kwa chanjo ya virusi vya corona katika miezi michache ijayo na hasa mwaka ujao.

Kauli hii ya Spahn inatolewa baada ya Taasisi ya Robert Koch nchini Ujerumani kukanusha ripoti ya awali kwamba kutakuwa na chanzo tayari katika msimu wa mapukutiko. Taasisi hiyo ilisema kwamba ripoti hiyo ilikuwa haijakamilishwa na ilichapishwa kimakosa.

Waziri Spahn hakutoa mwezi kamili ambao chanjo hiyo itakuwa tayari kwa sababu bado haijabainika ni mara ngapi watu watahitajika kupewa chanjo au kinga hiyo na itadumu kwa muda gani mwilini.

Waziri wa Utafiti wa Ujerumani, Anja Karliczek, awali alisema kwamba hakuna uwezekano wa chanjo yoyote kutolewa kwa umma kabla ya katikati ya mwaka ujao.

***DW***

## Ufaransa kuimarisha ulinzi mzozo gesi asilia

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, kuimarisha kwa muda uwapo wa jeshi la nchi hiyo katika eneo la Mashariki mwa Mediterenia kutokana na mzozo wa gesi asilia kati ya Uturuki na Ugiriki

Katika mawasiliano ya simu aliyofanya na Waziri Mkuu wa Ugiriki, Kyriakos Mitsotakis, Rais Macron alielezea wasiwasi wake kuhusu taharuki iliyoko katika eneo hilo.

Haya ni kwa mujibu wa taarifa kutoka makao makuu ya Rais huyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa, uwapo wa jeshi la Ufaransa utaimarishwa kwa muda katika siku zijazo ili kuangazia hali ilivyo katika eneo hilo na kuonyesha kujitolea kwa taifa hilo katika kuhakikisha uzingatiaji wa sheria ya kimataifa.

Hatua hii itachukuliwa kwa ushirikiano na mataifa washirika wa Umoja wa Ulaya ikiwa ni pamoja na Ugiriki.

Waziri Mkuu Mitsotakis aliishukuru jana Ufaransa kwa ahadi yake hiyo ya kuimarisha uwapo wa jeshi lake katika eneo la Mashariki mwa Mediterania ambapo meli za kivita za Ugiriki na Uturuki zinatishiana.

Zinatishiana kutokana na juhudi za Uturuki za utafutaji nishati katika sehemu ya bahari ambayo Ugiriki inadai kumiliki.

Katika ujumbe kupitia ukurasa wa twitter, Mitsotakis alisema kuwa Rais Macron ni rafiki wa kweli wa Ugiriki na pia mlinzi wa maadili ya bara la Ulaya na sheria za kimataifa.

Mapema wiki hii, Macron alitoa wito kwa Uturuki kusitisha shughuli hiyo ya utafutaji wa gesi katika eneo hilo la bahari linalozozaniwa hali ambayo imeongeza mvutano na Ugiriki.

Ufaransa ambayo ni mshiriki wa Ugiriki katika shirika la kujihami la NATO na pia katika Umoja wa Ulaya ni taifa lenye uwezo mkubwa zaidi wa kijeshi katika Umoja wa Ulaya.

Kufanya hali kuwa ngumu zaidi, Uturuki ambayo ni mpinzani mkubwa wa jadi wa Ugiriki katika kanda hiyo, pia ni mwanachama wa jumuiya ya NATO lakini haina uhusiano mzuri na Ufaransa.

***DW***

# NEYMAR:

## PSG HAIZUILIKI KUTWAA UBINGWA UEFA



**LISBON, Ureno**

NEYMAR amesema "haitawezekana" kuizuia Paris Saint-Germain kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kama wataendeleza morali yao ya kupambana hadi dakika ya mwisho baada ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Atalanta.

Mabingwa hao wa Ufaransa walikuwa wakielekea kutupwa nje kwenye mashindano hayo hatua ya robo fainali juzi Jumatano mjini Lisbon, baada ya kuwa nyuma kwa muda mrefu kwa bao la Mario Pasalic la kipindi cha kwanza.

Hata hivyo, Marquinhos alifunga bao la kusawazisha dakika ya 90 na Eric Maxim Choupo-Moting akafunga la ushindi sekunde 149 baadaye na kupindua matokeo hayo.

Licha ya kuonekana kuwa kwenye hatari ya kutolewa mikononi mwa Atalanta, Neymar amesisitiza hakuwa na hofu ya kuondolewa kwenye mashindano hayo.

"Kamwe sikufikiria kutolewa. Kamwe sikufikiria kurudi nyumbani," alisema akiiambia RMC Sport.

"Kuanzia mwanzo hadi mwisho, tulifikiria kuhusu kufuzu kwenye nusu fainali.

"Hakuna mtu aliyenibadilisha hilo, nataka kwenda kwenye fainali. Kiwango kingine kitakuja kwetu.

"Tuna furaha kubwa, tunapata uzoefu. Sisi ni kundi kubwa, familia na akili yetu inawaza kwamba, haiwezekani sisi kutolewa.

"Kamwe hatukukata tamaa, hata tukiwa kwenye mazingira magumu. Hamasa niliyonayo ni kushinda taji la Ligi ya Mabingwa na hiyo ilikuwa kwenye akili yangu kabla ya hata huu mchezo."

PSG imetinga nusu fainali ya mashindano hayo kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 1994-95, wakisubiri mshindi kati ya RB Leipzig au Atletico Madrid Jumapili, na Neymar anasubiri kwa hamu kubwa.

"Umebaki mchezo mmoja kwenda fainali. Tutapigana kwa kila kitu, tutafanya kila kitu kushinda," alisema.

"Ilikuwa ngumu. Atalanta ni timu kubwa, ambayo imecheza vizuri msimu mzima na imewashangaza wengi kwenye mashindano haya.

"Tulijua kwamba, tupo kwenye mstari mgumu, maana walikuwa wanacheza kwa kusukumiza mashambulizi kutoka kila upande wa uwanja."

## SANCHEZ HATIHATI NUSU FAINALI EUROPA

**DUSSELDORF, Ujerumani**

ALEXIS Sanchez anaweza asiwe fiti kwa ajili ya mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Ligi ya Europa, baada ya vipimo kuonyesha kwamba mshambuliaji huyo wa Inter Milan ameumia misuli.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile alifanyiwa matibabu kwenye mchezo wa robo fainali wa ushindi wa 2-1 dhidi ya Bayer Leverkusen mjini Dusseldorf Jumatatu na alimaliza mchezo huo huku akichechemea mguu wake wa kulia.

Katika taarifa iliyotolewa Jumatano, Inter ilithibitisha: "Alexis Sanchez amefanyiwa vipimo vya afya asubuhi mjini Duisburg baada ya kuumia kwenye mchezo dhidi ya Bayer Leverkusen.

"Vipimo vimeonyesha kwamba, ameumia misuli ya nyama za paja la kulia. Hali yake itaendelea kufuatiliwa kwa siku chake zijazo."

Inter itacheza na Shakhtar Donetsk, ambao waliwafunga Basel 4-1 kwenye hatua ya robo fainali, katika mchezo wa nusu fainali utakaopigwa mjini Dusseldorf, Agosti Jumatatu ijayo.

Sanchez mwenye umri wa miaka 31, amecheza mechi 30 kwa Inter msimu huu 2019-20.

Baada ya awali kujiunga kwa mkopo kutoka Manchester United, alisajiliwa moja kwa moja wiki iliyopita kutokana na kufikia makubaliano na 'Mashetani Wekundu' hao.

## SANCHO: NAPENDA KUCHEZEA DORTMUND

**DORTMUND, Ujerumani**

JADON Sancho amesema anapenda "kuichezea" Borussia Dortmund hasa kwa zao la wachezaji wa sasa baada ya kikosi chake hicho kuibuka na ushindi wa kuvutia wa mabao 6-0 kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Rheindorf Altach, Jumatano.

Mkurugenzi wa soka wa Dortmund, Michael Zorc, alibainisha mapema wiki hii kwamba, Sancho anayewaniwa na Manchester United, atabakia klabuni hapo kwa msimu wa 2020-21.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, Sancho, mwenye umri wa miaka 20, yupo na kikosi hicho kwenye kambi ya mazoezi nchini Uswisi na alicheza dakika 45 dhidi ya timu hiyo ya Austria, Altach, kwenye mchezo wao wa kwanza wa kirafiki wa maandalizi ya msimu mpya.



Lucien Favre aliweka sura nyingi mpya pamoja na Sancho kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Schnabelholz, kulekea msimu wake wa nne kwenye timu ya wakubwa, akifurahia na kizazi cha vipaji.

"Napenda kucheza sana hapa," alisema akiiambia BVB-TV. "Ni kundi maalumu. Tumepata wachezaji vijana wengi wanaochipukia. Kwa hakika nina furaha kubwa kucheza nao uwanjani.

"Mwanzo nilikuwa kama wao, nikicheza na wakubwa. Nafurahia kuwa nao."

## HABARI MICHEZO




# DE LIGT
## APASULIWA BEGA, NJE MIEZI MI3

**TURIN, Italia**

MLINZI wa Juventus, Matthijs de Ligt, anakabiliwa na uwezekano wa kukaa nje ya dimba kwa miezi mitatu baada ya kufanyiwa upasuaji wa bega.

Beki huyo wa kati wa Uholanzi alikuwa akisumbuliwa na tatizo la bega baada ya kuteguka mwaka jana.

Juve ilithibitisha Jumatano kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alifanyiwa upasuaji mjini Rome na operesheni hiyo ilikuwa na "mafanikio makubwa" na hataweza kuwa fiti hadi Novemba.

Bado haijawekwa wazi tarehe rasmi ya kuanza kwa msimu mpya wa 2020-21 katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A, lakini Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), awali lilibainisha kwamba inaweza kuanza Septemba Mosi.

De Ligt amecheza mechi 39 katika mashindano yote kwenye msimu wake wa kwanza na Juve tangu alipojiunga nayo kutoka Ajax kwa ada ya awali ya euro milioni 75 mwaka jana.

Juve walishinda taji la Ligi Kuu, Scudetto, kwa mara ya tisa mfululizo, lakini walifungwa na Napoli kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya Coppa Italia na walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora na Lyon.

Kocha Mkuu, Maurizio Sarri, alifukuzwa siku moja baada ya kutolewa kwenye mashindano hayo na akapandishwa aliyekuwa kocha wa kikosi cha Juve cha umri chini miaka 23 na kiungo wa zamani wa timu hiyo, Andrea Pirlo, kuwa kocha mkuu.

## CASILLAS KURUDI REAL MADRID

**MADRID, Hispania**




IKER Casillas amebainisha kwamba ana matumaini ya kurudi "nyumbani" pale Real Madrid, lakini si kucheza, hiyo ikija baada ya kupewa ofa na Rais wa klabu hiyo, Florentino Perez.

Gwiji huyo wa Hispania alitangaza kustaafu soka wiki iliyopita, akiwa hajacheza mchezo wowote tangu alipokumbwa na shambulio la moyo akiwa kwenye mazoezi na FC Porto, Mei Mosi, mwaka jana.

Casillas, golikipa alikulia kwenye akademi ya vijana ya Madrid na kucheza mechi 725 kwa klabu hiyo kabla ya kuondoka miaka mitano iliyopita, baada ya kukwaruzana na Rais Perez.

Hata hivyo, Casillas kwa sasa ana uhusiano mzuri na Perez na kipa huyo mwenye umri wa miaka 39, amethibitisha ripoti kwamba anaweza kurudi pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu kwa kazi ya ushauri.

"Hakuna kilichofungwa bado, lakini natumaini kwamba hatua yangu inayofuata nitakuwa pale Real Madrid," alisema akiliambia jarida la Semana.

"Kuondoka kutoka Real Madrid kulikuwa kwa mshituko, lakini ni nyumbani kwangu.

"Uhusiano wetu ulivunjika, kama ilivyo kwenye ndoa watu wanatengana na kusema kila kitu na kulikuwa na mambo mengi yaliyosemwa vibaya, lakini muda umepita na kila kitu kimetulia.

"Mwaka mmoja au miwili iliyopita, nilianza kuwa na uhusiano mzuri na Florentino na aliniambia mimi, 'unatakiwa kuwa hapa'.

"Sasa ni Agosti, tutazungumza kwa sababu Real Madrid ni nyumbani na ni maisha yangu. Florentino hivi karibuni alinipigia na kunipa ofa na sasa nitakaporudi Madrid, tutazungumza."



## JOAO FELIX ATAKA UFALME ATLETICO

**MADRID, Hispania**

NYOTA Joao Felix ana matumaini ya kufuata nyayo za Antoine Griezmann chini ya kocha, Diego Simeone pale Atletico Madrid.

Atletico ilitumia euro milioni 126 kumsajili mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ureno kutoka Benfica baada ya Griezmann kuondoka na kwenda Barcelona, ikizipiku klabu kadhaa zilizokuwa zinawania saini yake.

Umekuwa msimu wa kupanda na kushuka kwa Joao, ambaye amefunga mabao nane hadi sasa na kutoa pasi za mwisho tatu kwenye mechi 35 alizocheza katika mashindano yote.

Kiwango cha kupanda na kushuka kimechangiwa na majeraha msimu huu, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ana matumaini ya kuwa nyota mkubwa wa Atleti kama ilivyokuwa kwa Griezmann kabla yake.

"Kama nikiweza kufanya kile alichokifanya Griezmann au kujiimarisha zaidi, litakuwa jambo zuri kwa sababu ametengeneza historia na klabu hii," alisema Joao Felix akiliambia gazeti la Marca.

"Amefanya vizuri sana, amekuwa na El Cholo (Simeone), na kama nitafanya vizuri, litakuwa jambo bora sana kwake."


Baadhi ya wachambuzi wa soka wa Hispania wamekuwa wakikosoa staili ya Simeone anayotumia kumpanga Joao kwenye nafasi ya ushambuliaji.

Simeone mara kwa mara amekuwa akisisitiza Joao ataonyesha ubora wake mara tu atakapoizoea LaLiga, kitu ambacho Mreno huyo anakubaliana nacho.

"Watu wengi wanasema kitu kimoja, wengine wanasema kingine, lakini nipo hapa kucheza soka ambalo Cholo anataka nicheze," aliongeza.

"Subiri tuone. Naanza kuzoea soka la Hispania, na mara zote najifua kwa ajili ya kujiimarisha zaidi."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN: BARCA ITAITOA BAYERN LEO

Tumebakiwa na mechi tatu kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, nimejiandaa kwa kila kitu...

**LISBON, Ureno**

ANTOINE Griezmann anatarajia kuiona Barcelona ikitinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Agosti 23 na amebeba hadi "gemu yake ya PlayStation" kwa ajili ya kubakia hapo Lisbon.

Barca waliibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Napoli kwenye mchezo wa pili wa hatua ya 16-bora na kutinga robo fainali kwa ushindi wa uwiano wa mabao 4-2 na sasa watakutana na Bayern Munich leo Ijumaa kwenye dimba la Estadio da Luz.

Bayern imeshinda mechi 26 na kutoka sare moja katika mechi zake 27 za mashindano zilizopita na wanapewa nafasi kubwa ya kushinda taji hilo la Ulaya, lakini Griezmann amesema Barca wapo tayari kuwang'oa miamba hao wa Bavaria.

"Nimejiandaa kwa kila kitu katika begi langu tayari kubakia hapa Lisbon hadi Agosti 23 nimebeba pia gemu yangu ya PlayStation," alisema akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Tumebakiwa na mechi tatu kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini tuna nyenzo za kufanikisha hilo. Kila timu ina nafasi ya kushinda mchezo mmoja.

"Tunasubiri hilo, tumefanya kazi kubwa ya kiufundi na tupo tayari kucheza mchezo huu uliopo mbele yetu.

"Tunajua kwamba itakuwa ngumu, lakini tunajua nini tunachotakiwa kufanya ili kufuzu nusu fainali. Utakuwa mchezo mzuri sana.

"Tuna matumaini ya kufuzu kwa sababu ya ubora wa kikosi chetu. Tupo kwenye wakati mzuri na tunaweza kucheza mchezo mzuri sana.

"Tunatakiwa kuwa pamoja, mbele na nyuma, na kujaribu kuwa na mpira wakati wote kadili inavyowezekana."

## KWA UFUPI

**CITY YAJITOSA KWA ALCANTARA**

MANCHESTER City imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Bayern Munich, Thiago Alcantara na inaaminika imetoa ofa kubwa zaidi kuliko Liverpool kwa Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Sport-Bild - via Star)***

**UTD BADO IPO NA SANCHO**

MANCHESTER United imesimamisha kwanza suala la usajili kwa wachezaji wengine, huku wakijaribu kumsajili nyota wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Mirror)***

**JUVE YAMTAKA LACASETTE**

JUVENTUS imewasiliana na Arsenal juu ya uwezekano wa kumsajili straika wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29. ***(CalcioMercato)***

**WATFORD: BEI YA ISMAILA HII**

WATFORD inataka ada ya zaidi ya pauni milioni 40 kwa winga wake, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 22 raia wa Senegal, wakati Liverpool na klabu nyingie Ulaya zikionyesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Evening Standard)***

**ROMA YAMUWANIA TORREIRA**

AS Roma inaweza kumtoa kiungo wa kimataifa wa Guinea, Amadou Diawara mwenye umri wa miaka 23 ili kumpata kiungo wa Arsenal, Lucas Torreira (24), raia wa Uruguay. ***(Gazzetta dello Sport - via Mail)***

**GREALISH KUKALISHWA VILLA**

JACK Grealish atafanya mazungumzo maalumu na Ofisa Mtendaji wa Aston Villa, Christian Purslow wakati akirudi kutoka likizo, huku Manchester United bado ikiwa inamuwania kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24 raia wa Uingereza. ***(Mirror)***

**BENFICA YAMTAKA VERTONGHEN**

BENFICA inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Tottenham, Jan Vertonghen na nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Ubelgiji, anaweza kujiunga na klabu hiyo kuungana na mchezaji wa Uruguay na straika wa zamani wa Paris St-Germain, Edinson Cavani mwenye miaka 33. ***(Sun)***

**CITY, ARSENAL KWA AOUAR**

MKURUGENZI wa michezo wa Lyon, Juninho, amesema kiungo, Houssem Aouar anaweza kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto, huku Arsenal, Manchester City na Juventus zote zikimfuatilia Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

**POGBA, UNITED KUTETA**

KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, anatarajia Manchester United kufungua mazungumzo mara tu mashindano ya Ligi ya Europa yatakapomalizika. ***(Sky Sports)***

**PICKFORD AITESA EVERTON**

KLABU ya Everton inaweza kutafuta mrithi wa Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 26, wakati kocha Carlo Ancelotti anahisi kwamba golikipa huyo Muingereza hana uwezo wa kutosha. ***(Star)***

**ARSENAL YAMULIKA SPORTING**

ARSENAL inawania kumsajili kinda la Sporting Lisbon, Joelson Fernandes mwenye umri wa miaka 17. Nyota huyo wa kikosi cha timu ya Taifa ya Ureno chini ya umri wa miaka 17, amekuwa akitajwa kama 'Cristiano Ronaldo' mpya. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# NDAYIRAGIJE, AUSSEMS WAWAGAWA YANGA SC

**Na Faustine Feliciane**

MCHAKATO wa kumsaka kocha mkuu wa Yanga bado umeonekana kuwa suala gumu kuamuliwa na wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo huku majina mawili, Mrundi Etienne Ndayiragije na Mbelgiji Patrick Aussems yakiwagawa, imefahamika.

Mpaka sasa Yanga imeeleza ina majina ya makocha zaidi ya 50 ambao wameomba kukifundisha kikosi hicho, lakini majina yanayoongoza katika mbio hizo ni la Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Ndayiragije na aliyekuwa Kocha wa Simba, Aussems.

Taarifa kutoka chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, zimeeleza wajumbe wamegawanyika kuhusu uamuzi wa nani apewe nafasi ya kuifundisha timu hiyo.

"Wapo wanaompa nafasi Ndayiragije, lakini wengine wanataka apewe Aussems ambaye amepata mafanikio makubwa katika ngazi ya klabu akiwa na Simba, bado tunaendelea na majadiliano, lakini ndani ya kipindi kifupi klabu itatangaza kocha tutakayeafikiana kumpa kazi," kilieleza chanzo chetu.

Aidha, kilisema licha ya kuwapo kwa majina hayo mawili bado wanaangalia na sifa za makocha wengine walioomba kazi ya kufundisha timu hiyo.

Alipoulizwa Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Fredrick Mwakalebela kuhusu mchakato huo, alisema: "Mchakato bado unaendelea, pindi mambo yatakapokamilika basi kila kitu kitawekwa wazi." Alisema majina yaliyopo mezani ni mengi zaidi ya hayo mawili (Aussems na Ndayiragije) na wanaendelea kuyachambua kupata mtu sahihi wa kuifundisha timu hiyo.

Yanga inasaka kocha mpya baada ya kumtimua aliyekuwa Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Aymael na kuvunja benchi lote la ufundi huku wakimbakisha kocha wa viungo, Riedoh Berdien na kumpandisha kocha wa timu ya vijana, Said Maulidi kusaidiana naye.

MABINGWA...




Wachezaji wa Simba Queens, wakisherehekea ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake msimu wa 2019/20 walipokabidhiwa juzi baada ya mechi yao ya funga msimu dhidi ya TSC Queens iliyopigwa katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza na kushinda kwa mabao 9-0.
**PICHA: SIMBA**

# Humud amwaga wino Namungo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo imeendeleza dhamira yake ya kukiimarisha kikosi chake baada ya kumsajili kiungo mzoefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Abdulhalim Humud kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Mtibwa Sugar.

Mtandao wa Klabu ya Namungo umethibitisha kumsajili kwa miaka miwili mchezaji huyo anayecheza nafasi ya kiungo mkabaji huku wakimkabidhi rasmi jezi ya timu hiyo.

Huyo ni mchezaji wa tatu mpya kusajiliwa na klabu hiyo, baada ya kumsajili mchezaji wa Lipuli FC ambayo imeshuka daraja, Fred Tangalo anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, pamoja na straika kutoka nchini Ghana, Steven Sey, ambaye alikuwa anaichezea Singida United iliyoshuka daraja.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, alisema mchakato wa usajili unaendelea kutokana na mapendekezo ya Kocha Mkuu, Hitimana Thiery, na kwamba pamoja na usajili huo wanatarajia kusajili pia golikipa mwenye kiwango cha juu.

"Usajili unaendelea, tunasajili kwenye upungufu na nafasi ya golikipa ambayo pia tunaitazama na tutasajili mwenye uwezo mkubwa," alisema Zidadu.

Kwa sasa Namungo ina kipa Mghana Nurdin Barola ambaye kwa sasa anatafutiwa kipa mwingine bora ili kumpa changamoto.

Mbali na hilo, alisema wapo kwenye hatua za mwisho kusajili mchezaji wa kimataifa kutoka nchini Uganda ambaye hakutaka kumtaja jina.

"Tunaongea na mchezaji mmoja kutoka nchini Uganda, mambo yakikamilika kila kitu kitakuwa wazi," alisema Mwenyekiti huyo.

Namungo itaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika (Caf), huku Simba ikipeperusha bendera ya nchi katika michuano ya Ligi ya Mabingwa.

## Simba Queens yanogesha ubingwa

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kwamba tayari kilishajihakikishia ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake kutokana na kufikisha pointi 53 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote, Kikosi cha Simba Queens, kimefunga msimu wa ligi hiyo kwa kutoa kipigo cha mbwa mwizi baada ya kuichapa TSC Queens kwa mabao 9-0 katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza juzi.

Katika mechi hiyo ambayo baada ya kumalizika Simba Queens ilikabidhiwa kombe kwa kuwa mabingwa kwa msimu wa 2019/20, mabao yake yalifungwa na Asha Djafar, Opah Clement aliyeondoka na mpira kutokana na kutupia hat-trick, Joele Bukuru aliyefunga mawili pamoja na Mwanahamisi Omary aliyecheka na nyavu mara mbili. Hat-trick hiyo, inamfanya Oppah Clement kumaliza msimu akiwa na mabao 20 nyuma ya mshambuliaji wa JKT Queens, Fatma Mustaf aliyeondoka na Kiatu cha Dhahabu kwa kuwa mfungaji bora wa ligi hiyo baada ya kucheka na nyavu mara 30 kabla ya mchezo wao wa juzi.

Simba Queens imemalizika ligi hiyo ikiwa na pointi 56 baada ya kucheza mechi 22 huku tofauti ya mabao yao ya kufunga na kufungwa yakiwa ni 69.

## Ihefu FC: Ukimya una kishindo kikuu

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa Ihefu FC, Juma Nyauba, amesema ukimya wao una kishindo kikubwa ambacho timu hiyo itaonyesha katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nyauba alisema mambo yao wanafanya kimya kimya ikiwamo usajili kwa ajili ya kukiimarisha kikosi cha timu hiyo kwa msimu wao wa kwanza Ligi Kuu Bara.

Alisema wako makini katika usajili wao kuhakikisha wanapata wachezaji wazuri watakaosaidia timu yao hiyo kufanya vizuri katika michezo yote ya nyumbani na ugenini.

"Tuko katika mazungumzo na baadhi ya wachezaji kutoka timu za Ligi Kuu na Daraja la Kwanza, kupitia mapendekezo ya benchi letu la ufundi kuhakikisha tunaboresha kikosi cha timu yetu kwa msimu mpya," alisema Nyauba.

Mwenyekiti huyo alisema wamekuja kuleta changamoto katika soka kwa kuhakikisha wanajipanga kusajili vizuri wachezaji watakaofikia malengo yao ya kumaliza ligi hiyo katika nafasi nzuri.

Ihefu imepanda kucheza Ligi Kuu baada ya kufanya vizuri katika mechi zake za mchujo kwa kuitoa Mbao FC ya Mwanza.

Michezo
Ijumaa Agosti 14, 2020
Nipashe




## Griezmann: Barca itaitoa Bayern leo

HABARI UK 22




Bernard Morrison, akisaini mkataba wa kuichezea Simba kabla hukumu ya kesi yake na Yanga kutolewa juzi: PICHA: Simba

# MASWALI MA5 MAGUMU HUKUMU YA MORRISON

**Wanasheria wachambua udhaifu uliopo, TFF kimya, lakini yahusishwa kwa...**

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kutoa hukumu kwa kumpa ushindi kiungo Mghana Bernard Morrison dhidi ya klabu yake ya Yanga, hukumu hiyo imeacha maswali magumu kwa mashabiki na wadau wa soka, lakini pia kwa Watanzania wote kwa ujumla.

Katika kesi ya msingi iliyokuwa ikisikilizwa na kamati hiyo, ilikuwa ni dhidi ya mlalamikaji, Morrison ambaye alidai mkataba wake na Yanga ni wa miezi sita na umekwisha muda wake na kwamba mkataba mpya wa miaka miwili anaodaiwa kuingia na klabu hiyo si halali kwa kuwa saini yake imeghushiwa.

Kamati hiyo ikiwa chini ya Mwenyekiti wake, Elias Mwanjala ilijifungia kwa siku tatu ikijadili, kupitia nyaraka mbalimbali na mkataba huo pamoja na kuwahoji wahusika kuanzia Agosti 10 kabla ya juzi jioni kutoa hukumu kwa kumtangaza Morrison kushinda.

Hata hivyo, kinachowasumbua wadau wa soka hususan wabobezi wa sheria si ushindi kwa Morrison, bali ni vipengele vilivyotumika kumtangaza mshindi hasa ikizingatiwa kesi ya msingi iliyokuwa mbele yao ilikuwa ni mchezaji kulalamika si yeye amesaini mkataba husika, lakini katika hukumu iliyosomwa na Mwanjala ikaeleza mkataba kutokuwa halali kutokana na baadhi ya upungufu.

Akisoma hukumu hiyo, Mwanjala alisema: "Tumekuwa makini katika kufuata haki na kamati yetu ilikuwa makini, kulikuwa na mapungufu makubwa upande wa tarehe ambapo kuna sehemu ilionyesha kuwa amesaini Machi 20 huku chini ikionyesha Julai 15, 2020.

"Pia kuna ukurasa wa saini kwenye mkataba unaoonyesha kuna upungufu katika sehemu ya saini ambayo imefutwa kwa kalamu jambo ambalo linaonyesha kwamba kulikuwa kuna tatizo kwenye masuala ya mkataba, ni upungufu mkubwa, hivyo tunampa ushindi Morrison anakuwa mchezaji huru, suala la timu atakayocheza itakuwa ni uamuzi wake."

Maswali Magumu

Ikumbukwe baada ya hukumu hiyo, Morrison amepelekwa kwenye Kamati ya Nidhamu ya TFF kutokana na kitendo chake cha kusaini mkataba na Simba wakati kesi yake ilikuwa bado haijatolewa uamuzi, na aliyempeleka huko ni Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ambayo ni kubwa zaidi. Je, kwa nini irudishe tena chini?

Pili, je, saini inaweza kuondoa uhalali wa mkataba huo kama mambo mengine ya msingi yalikuwapo kwenye mkataba?

Tatu, kama suala lilikuwa tu upungufu wa saini kukatwa na tarehe, je walipaswa kutumia siku tatu kulibaini hilo?

Nne, ni nyaraka gani Mwanjala aliwaeleza waandishi wa habari siku ya pili kuwa amewaagiza Yanga na Morrison kuzipeleka?

Tano, je mkabata huo ulishafikishwa TFF, kama ndivyo, iliukagua? Na kama iliona kuna upungufu huo kwa nini isiwatake wahusika kuyarekebisha kwanza?

Maswali hayo yamewafanya wadau kuwa na mashaka kwamba kuna kilichopo nyuma ya pazia, kwa TFF yenyewe kuvurunda hivyo kuficha udhaifu wake ama Yanga pengine ilighushi hivyo kutaka kuinusuru au huenda kuna upande wenye maslahi na Morrison umechangia kutolewa kwa uamuzi hao.

Mwanasheria na mdau mkubwa wa soka nchini ambaye pia alikuwa akiitetea Yanga kwenye shauri hilo, Alex Mgongolwa, aliliambia Nipashe: "Tarehe na saini peke yake hakuwezi kuufanya mkataba kutokuwa halali, mtu anaweza akaingia mkataba leo lakini mkataba huo ukaanza kufanya kazi tarehe za mbele, lakini pia kama kuna makubaliano yalifikiwa na mambo yote ya msingi yakafanyika ikiwa ni pamoja na malipo stahiki."

Aidha, Naibu Waziri wa zamani wa Michezo, Mudhihir Mudhihir, ambaye pia ni mwanasheria kitaaluma, alihoji kama mkataba ulikuwa na upungufu kwa nini Morrison amepelekwa kwenye kamati ya nidhamu.

"Pamoja na kwamba mimi ni Yanga, nikiweka pembeni U-yanga wangu, nadhani kamati imepotoka kidogo kwenye sheria, kama ni tarehe tu na saini bado hakuwezi kuufanya mkataba huo kuwa batili ikiwa kuna makubaliano mengine ya msingi yamefikiwa na yanaonekana kwenye mkataba," alisema Mudhihir.

Lakini mapema TFF ilipoulizwa kama mkataba huo wenye upungufu kwa mujibu wa kamati hiyo, ulishafikishwa kwao, haikutaka kueleza chochote na badala yake ikamtaka mwandishi wetu kuwasiliana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwanjala.

Msemaji wa TFF, Clifford Ndimbo alisema: "Ni vigumu sisi (TFF) kuzungumzia suala hilo, ni vema akapigiwa mwenyekiti wa kamati aelezee kuhusu hilo, itaonekana kila mtu analizungumzia wakati ni jambo la kamati," alisema Ndimbo.

## SIMBA KUANIKA NYOTA WAPYA LEO

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema leo utaanza rasmi kuwatambulisha silaha zao mpya akiwamo Bernard Morrison ambaye ni miongoni mwa nyota waliosajili kukitumikia kikosi hicho kuelekea msimu wa 2020/21.

Mbali na Morrison, Simba tayari imewasajili mabeki, Ame Ibrahim (Coastal Union), David Kimeta (Lipuli) pamoja na mshambuliaji wa KMC, Charles Ilanfya.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alisema utambulisho wa wachezaji hao utajumuisha pamoja na wiki yao ya Simba kwa kuipa jina la 'Wiki ya Mabingwa 2020' ambayo kilele chake ni Agosti 22 mwaka huu.

"Mbali ya kutambulisha wachezaji pia tutatambulisha nembo mpya ambayo tumeifanyia maboresho, lakini pia tutazindua jezi zetu zitakazotumikia msimu mpya wa 2020/21, huku Jumapili tukisoma dua kuombea waliotangulia mbele za haki.

"Baada ya hapo kwa kushirikiana na mdhamini wetu SportPesa tutatembelea timu za mtaani kuunga mkono soka la vijana kwa kutoa vifaa kwa vijana hao," alisema Manara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >